CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO (CHADEMA)



ILANI YA UCHAGUZI MKUU WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI,

OKTOBA 31, 2010

Agosti 2010

YALIYOMO

DIBAJI **5**

SURA YA KWANZA **10**

1. MISINGI YA SERA ZA CHADEMA **10**

SURA YA PILI **13**

2. FURSA KWA KILA MTOTO WA KITANZANIA KUPATA ELIMU BORA **13**

2.1 Utangulizi 13

2.2 Hali halisi kuhusu elimu hapa nchini 13

2.3 CHADEMA itafanya nini? 17

2.3.1 Kuhusu Elimu ya Msingi na Sekondari 18

2.3.2 Kuhusu Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu 21

SURA YA TATU **25**

3. FURSA KWA KILA MTANZANIA KUPATA HUDUMA BORA ZA JAMII **25**

3.1 Utangulizi 25

3.2 Afya 25

3.2.1 Hali halisi kuhusu huduma za afya hapa nchini 25

3.3 CHADEMA itafanya nini kuhusu afya? 26

3.4 Maji 30

3.4.1 Hali halisi ya huduma za maji nchini 30

3.4.1 CHADEMA itafanya nini kuhusu maji? 31

3.5 Uendelezaji makazi na nyumba 31

3.6 Huduma kwa watu wenye ulemavu 33

3.6.1 Hali halisi ya huduma kwa watu wenye ulemavu nchini 33

3.6.2 CHADEMA itafanya nini? 34

SURA YA NNE **37**

4. KUJENGA KILIMO BORA NA CHA KISASA **37**

4.1 Utangulizi na hali halisi ya kilimo hapa nchini 37

4.1.1 CHADEMA itafanya nini kuboresha kilimo? 38

4.1.2 Mipango Mingine Kuhusu Kilimo na Mifugo 42

SURA YA TANO 44

5. FURSA KWA KILA MTANZANIA KUJENGA NA KUMILIKI UCHUMI IMARA NA SHIRIKISHI 44

5.1 Utangulizi 44

5.2 Hali halisi kuhusu uchumi wetu 45

5.3 Nishati 47

5.3.1 Hali halisi ya nishati nchini 47

5.4 Madini 47

5.4.1 Hali halisi ya madini nchini 47

5.5 CHADEMA itafanya nini kuboresha na kuimarisha uchumi? 49

5.5.2 Mpango wetu maalumu wa ‘kumijishisha’ vijiji 51

SURA YA SITA 54

6. KUJENGA UONGOZI BORA NA MFUMO MPYA WA UTAWALA 54

6.1 Utangulizi 54

6.4 CHADEMA itafanya nini katika kujenga uongozi bora na kuimarisha utawala wa sheria? 56

SURA YA SABA 60

7. FURSA KWA KILA MTANZANIA KUPATA AJIRA, UJIRA BORA, MFUMO WA PENSHENI NA HUDUMA KWA WAZEE 60

7.1 Utangulizi 60

7.2 CHADEMA itafanya nini kukuza ajira na ujira bora? 61

7.2.1 Kuhusu ajira na ujira bora 61

7.2.2 Kuhusu mfumo wa pensheni na huduma kwa wazee 62

SURA YA NANE 66

8. KUIMARISHA ULINZI NA USALAMA 66

8.1 Utangulizi na hali halisi 66

8.2 CHADEMA itafanya nini katika kuimarisha ulinzi na usalama? 67

8.2.1 Jeshi la Polisi 67

8.2.2 Jeshi la Magereza 70
8.2.3 Kikosi cha Uokoaji 71
8.2.4 Idara ya Uhamiaji 72
8.2.5 Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa 73
8.2.6 Idara ya Usalama wa Taifa 75
SURA YA TISA **77**
9. KUKUZA NAFASI YA TANZANIA KATIKA DIPLOMASIA YA KIMATAIFA **77**
9.1 Utangulizi 77
SURA YA KUMI **79**
10. KUINUA NA KUKUZA SANAA, MICHEZO NA UTAMADUNI **79**
10.1 Utangulizi 79
10.2 Sanaa 79
10.3 Michezo 81
10.4 Kuunda Kamisheni Maalumu ya Rais ya Historia ya Tanzania 84
SURA YA KUMI NA MOJA **85**
11. VIPENGELE MAALUM **85**
11.1 Zanzibar na Muungano 85
11.2 Unguja 85
11.3 Pemba 86
11.4 Mpango wa CHADEMA kuhusu Wanawake na Watoto 87
11.5 Kujiandaa kwa Majanga 88
HITIMISHO: ILANI YA MABADILIKO **90**

DIBAJI

Tanzania inahitaji mabadiliko ya haraka ya uongozi wa nchi yetu, mfumo wake wa utawala, mtazamo na mwelekeo wa watu wake na mabadiliko katika utendaji wa kazi mbalimbali ili hatimaye kama Taifa tuweze kupiga hatua ya haraka, ya uhakika na ya makusudi kutoka kuwa miongoni mwa nchi maskini zaidi duniani na kuwa nchi ya maendeleo ya juu duniani. Bila ya mabadiliko hayo yatakayosimamiwa vizuri, Tanzania itaendelea kuwa nchi inayoishi kwa matamanio ya mafanikio huku ikiendelea kuishi katika umaskini wa kutupa ilihali kikundi kidogo cha watu wakiendelea kujinufaisha kwa mgongo wa taifa hili.

Nchi yetu imejaliwa utajiri mwingi, ikiwemo maliasili maridhawa kama madini, mbuga za wanyama, pwani nadhifu na za kuvutia, gesi asilia (yenye kuashiria uwepo wa mafuta) ndege na wanyama wa kila aina wa kufugwa na wa mbugani! Aidha, nchi yetu imejaliwa raslimali watu, wenye akili, vipaji vya kila aina, wenye bidii ya kazi, wapole na wapenda amani. Hata hivyo, Watanzania wamebaki maskini wa kutupwa, na umaskini huu unaendelea kuongezeka kila kukicha. Miaka minne iliyopita wakati Rais Kikwete akiomba kuchaguliwa kuwa Rais, yeye na chama chake cha Mapinduzi waliahidi kuumaliza umaskini na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Hata hivyo, katika kipindi cha utawala wa Rais Kikwete, watu milioni 2 wamekuwa maskini zaidi na kufanya idadi ya Watanzania walio maskini wa kutupwa kufikia milioni 13! Badala ya kutengeneza mazingira na mfumo wa utawala na utendaji ambao ungetoa nafasi ya maisha bora kwa kila Mtanzania, viongozi wa CCM na serikali yao wameendeleza mfumo ule ule mbovu ambao umewahakikishia wao wenyewe, ndugu, jamaa na marafiki zao maisha bora huku Watanzania walio wengi wakiendelea kuwa maskini.

Hivi karibuni Rais wetu, Jakaya Mrisho Kikwete, aliulizwa na waandishi wa habari wa Jijini Paris, Ufaransa kwamba “Nchi yako ina utajiri mkubwa wa maliasili, inakuwaje Watanzania ni masikini wa kutupwa?” Alijibu, kwa furaha na kwa kujiamini, ***“Hata mimi sijui sababu; ninajiuliza kila siku swali hilo lakini sijapata jibu!’’*** Huyo ndio dereva wa gari tulilopanda; hajui anakotoka wala aendako. Sote tunaelewa hatari ya

kupanda gari ambalo dereva wake hajui anapoenda. *Kama Rais wa nchi hajui sababu kwa nini nchi yetu ni maskini atawezaje kupambana na huo umaskini?* Hata hivyo, CHADEMA hatuamini kwamba Rais Kikwete hajui chanzo cha umaskini katika nchi yetu. Rais Kikwete anajua chanzo cha umaskini wa nchi yetu lakini hawezi kukitaja kwa kuwa yeye mwenyewe ni sehemu ya tatizo hilo.

Kuna sababu tatu zilizosabisha nchi yetu ifike hapa ilipo, nazo ni: ***ufisadi, ufisadi*** na ***ufisadi***. Ufisadi ndio tishio kubwa kabisa la mustakabali wa nchi yetu. Ndio kusema tukitaka tutoke hapa tulipo ni lazima tuukatae na tupambane na ufisadi.

Ufisadi ni nini?

Tunapozungumzia Ufisadi tunazungumzia mfumo na muundo wa utawala ambao umetengeneza utamaduni wa kuishi kiujanja ujanja, matumizi mabaya ya madaraka na vyeo, ufujaji wa mali ya umma, wizi wa fedha za umma, utaratibu wa kubebana na ajira zinazotegemea kujuana, na mahusiano ya watawala na watawaliwa ambayo msingi wake ni woga, vitisho, na kujiona watu wanastahili zaidi kuliko wengine. Ni mfumo uliodidimiza tawala mbalimbali duniani na ambao pasipo kuushughulikia kwa makusudi unasimama kama tishio lilopo na la hatari kwa Tanzania kuliko vita. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere alisema kuwa “ufisadi na rushwa ni adui mkubwa zaidi wa maslahi ya wananchi wakati wa amani kuliko vita” (Bungeni, Mei 17, 1960, kikao cha 35 cha bajeti).

Ufisadi ndio kizuizi kikubwa cha kuboresha maisha ya watu wetu; ni kikwazo kikubwa katika kujenga na kuimarisha utawala bora, utawala wa sheria na haki za raia. Ufisadi ndio kikwazo kikubwa kabisa cha maendeleo ya nchi. Ndio kusema, juhudi zetu za kujiletea maendeleo kama nchi haziwezi kufanikiwa bila kwanza kukomesha ufisadi.

Tumekuwa na miaka takribani 50 ya CCM. Wameahidi kila aina ya ahadi na wamefanya kila makosa, lakini tukawavumilia na tukawapa nafasi nyingine tukiamini kwamba mambo yatabadilika. Kila tulipowapa nafasi, hali ilizidi kuwa mbaya, tukasogea kutoka kubaya kwenda kubaya zaidi. Lengo lao kubwa limekuwa ni kushinda uchaguzi, ili

waendelee kutumia madaraka tunayowapa kwa ajili ya kujinufaisha kwa njia ya ufisadi. **Ni wakati wa mabadiliko, na fursa ya kufanya mabadiliko ni huu uchaguzi wa 2010 na siyo 2015**. Tukisubiri wakati mwingine tutakuwa tumechelewa sana. Na tukiwapa nafasi nyingine moja CCM ya kututawala tena tutakuwa tumewapa leseni ya kuendelea kutawala wapendavyo na tutakuwa tumejihukumu sisi wenyewe na uzao wetu katika maisha ya umaskini wa kudumu.

Hivyo basi, lengo kuu la CHADEMA katika ilani hii kuelekea Uchaguzi Mkuu ni kuhuisha uzalendo, maadili na uadilifu katika uongozi wa nchi ambao ndio msingi mama wa kukomesha ufisadi. CHADEMA inaamini kwamba ili tuweze kutoka hapa tulipo panahitajika uongozi wenye maono ya kizalendo, adilifu, makini na wenye upeo, ambao utasimamia kikamilifu utafutaji na uvunaji wa raslimali za nchi kwa manufaa ya nchi na watu wake. Viongozi wa CHADEMA wameonyesha kwa kauli na matendo yao kuwa ni wenye maono na wazalendo, adilifu, makini na wenye upeo. Kazi tuliyoifanya kama chama cha upinzani ndani na nje ya Bunge Watanzania wameiona. Tumefanikiwa kuwaumbua mafisadi wanaoifilisi nchi yetu na ambao wamefunga fungate na Serikali ya CCM. Hata hivyo, pamoja na kwamba kuwaumbua mafisadi ni hatua muhumu, haitoshi kuutokomeza ufisadi. Ili kuutokomeza ufisadi panahitaji uongozi makini serikalini wenye uwezo na kusudio lisilo na utata la kuutokomeza mfumo wa kifisadi katika hali zake zote ili kurejesha uadilifu na uaminifu katika utumishi wa umma na mfumo wetu wa utawala. Muhimu zaidi, panahitajika uongozi ambao sio sehemu ya genge la mafisadi.

Hivyo basi, ili kuutokomeza ufisadi hapa nchini tunahitaji mabadiliko ya makusudi ya uongozi kuanzia ngazi ya madiwani, Ubunge na Urais ili kuipa nchi nafasi ya kuanza upya ujenzi wa Taifa letu. CHADEMA tupo tayari kuongoza vita dhidi ya ufisadi na kuleta mabadiliko yanayostahiki kwa nchi hii pasipo kumuonea mtu, kumbeba mtu au kumwonea haya au woga mtu yeyote. Kwetu Tanzania iko juu ya cheo, hadhi au jina la mtu yeyote. Tunaomba Watanzania wote tuwe sehemu ya mabadiliko tuyatakayo kwa kuichagua CHADEMA katika uchaguzi huu.

Ilani hii inaanisha maeneo na vipaumbele vitakavyozingatiwa na CHADEMA mara itakapopata nafasi ya kuunda serikali. Serikali ya CHADEMA inalenga katika kujenga

uchumi imara na shirikishi na kuunda serikali ndogo yenye kuzingatia maadili, ufanisi, uzalendo na nidhamu katika matumizi ya fedha. Tutabadili mfumo wa utawala kutoka utawala wa hofu kwenda utawala wenye matumaini. Tutaelekeza fedha za walipa kodi na raslimali za taifa kwenye kuboresha mashule, kuboresha maslahi ya walimu na wafanyikazi, kuboresha afya za Watanzania na kujenga miundo mbinu imara kwa ajili ya kukuza uchumi. Katika kutekeleza haya tutajikita katika kutokomeza wimbi la ufisadi lililoasisiwa na kulindwa na CCM na Serikali yake. Tofauti na Serikali ya CCM inayojivunia kusifiwa na watu wa nje hata kama mamilioni ya wananchi wanalia, tutazingatia mahitaji ya Wananchi kwanza kuliko mahitaji ya wageni kwa sababu tunaamini kuwa siasa sahihi ni kujali wananchi.

Kwa mara nyingine tena, kupitia uchaguzi huu, Watanzania tunakumbushwa wajibu wetu wa kikatiba na kitaifa. Tunao wajibu wa kuhakikisha kuwa tunachagua viongozi wanaozingatia maslahi ya Taifa na watakaosimamia uhai na ustawi wa nchi yetu kwa manufaa ya kizazi cha leo na kijacho. **Kuchagua CHADEMA ni kuchagua mabadiliko na kukataa ufisadi**. CHADEMA tunaamini kuwa *Mabadiliko ya kweli hayawezi kuletwa na mafisadi wale wale, wa chama kile kile, wakiendeleza yale yale, kwa ari, nguvu na kazi(anguka) zaidi*.

Ilani hii sio ahadi, ni mpango wa kazi ambao tutautekeleza kama CHADEMA itapatiwa na wananchi ridhaa na nafasi ya kuongoza. Kwa ufupi, Ilani hii itakayobeba mwelekeo wa CHADEMA kama chama tawala kuanzia 2010-2015 ina lengo la kuomba ridhaa ya wananchi ili tuweze kuanza tena ujenzi wa taifa letu jukumu ambalo CCM imeliacha kwa miaka zaidi ya ishirini sasa. Tunataka kurudia jukumu la kwanza kabisa la taifa letu baada ya Uhuru na Muungano yaani kujenga Taifa la kisasa. Kama Baba wa Taifa alivyosema **“maendeleo ni ya watu siyo vitu”** tunaamini kabisa kuwa tukirudisha maono yenye kulenga maendeleo ya watu basi maendeleo ya vitu yataenda sambasamba kabisa na maendeleo ya watu hao.

Ilani hii ni dira na ni maono yenye kuthubutu. Ni dira ya kutupeleka tunakotaka kwenda kwa ufanisi mkubwa na kwa muda mfupi zaidi na ni maono ya Tanzania gani tunayoitaka

kuanza kuijenga ndani ya miaka hii mitano. Hii ni Ilani ya Mabadiliko, ni Ilani ya Matumaini, ni Ilani ya kimapinduzi.

Hivyo basi, hii ni nafasi yako ya pekee ya kuamua kuirudisha serikali yako mikononi mwako kwa kuipa CHADEMA nafasi ya kushika hatamu ya uongozi wa Taifa ili kwa pamoja tuweze kujenga Taifa la kisasa, lenye watu wenye nafasi sawa ya kufanikiwa, na lenye matumaini kwa watu wake sasa hivi na uzao wao baadaye.

Kama unaamini mabadiliko ya kweli yanatakiwa kuanza sasa hivi, na endapo uko tayari kuungana nasi katika kuyaleta mabadiliko hayo basi ni uchaguzi mmoja tu umebakia mikononi mwako:

Chagua CHADEMA, Tumaini Jipya!

Chagua Rais Dk Wilbroad Slaa kutoka CHADEMA

Chagua Wabunge kutoka CHADEMA

Chagua Madiwani kutoka CHADEMA

Twende tukajenge Taifa letu, pamoja tunaweza!.

Dkt. Wilbroad Peter Slaa,

Mgombea Urais CHADEMA 2010.

SURA YA KWANZA

1. MISINGI YA SERA ZA CHADEMA

Uchaguzi huu lazima uwe ni uchaguzi wa mabadiliko kwa Tanzania. Ni uchaguzi muhimu unaopaswa kuwa mwanzo wa safari ya kuleta mabadiliko ya kweli na uhuru wa kweli. Ili tuweze kuleta mabadiliko ya kweli, kuna mambo mawili ya msingi ya kuzingatia.

Mosi, ni muhimu tuelewe na tuwe wa kweli juu ya chanzo cha matatizo yetu na ni kwa namna gani tumefika hapa tulipo leo. CHADEMA tunaamini kwa dhati kuwa tatizo mama lililotufikisha hapa tulipo ni ***ufisadi uliosababishwa na uasi wa viongozi dhidi ya misingi mama ya utanzania ambayo ni: uzalendo na uadilifu***. Hivyo basi, hatua ya kwanza ya kutoka hapa tulipo ni ***kuushugulikia kwa haraka ufisadi kwa kurudisha na kuhuisha uzalendo na uadilifu katika uongozi wa nchi***. Na hili ndilo litakuwa lengo kuu la utendaji wa Serikali itakayoundwa na CHADEMA kuanzia Novemba 1, 2010.

Pili, Watanzania tutambue kwamba tukiamua kwa dhati na kuchukua hatua katika uchaguzi huu wa 2010 tuna uwezo wa kubadili hali tuliyo nayo kutoka taifa linaloendelea taratibu na kuwa taifa linaloendelea kwa kasi. Uchaguzi huu ni nyenzo muhimu na ya pekee ya kuweza kubadili hali ya nchi yetu na kurudisha matumaini kwa Watanzania wote bila kujali hali, itikadi, rangi, kabila, dini au kitu kingine chochote ambacho kinaweza kuwatofautisha mmoja mmoja.

Mafanikio mbalimbali yaliyopatikana tangu nchi yetu ipate uhuru katika sekta mbalimbali ikiwemo elimu, afya, miundo mbinu na uchumi, bado hayaendani kabisa na hali halisi ya umri wetu kama nchi na raslimali ambazo nchi imejaliwa. Watanzania walio wengi wanaendelea kuwa maskini wa kutupwa, ndani ya nchi tajiri kupindukia kwa raslimali za aina zote. Familia nyingi zinahangaika kupata mlo moja. Shule za umma zimetelekezwa (bado kuna maelfu ya watoto wetu wanaokaa kwenye matofali na kwenye mavumbi), walimu wanadhalilishwa kiasi hata cha kuchapwa viboko, na hakuna wa kuwatetea. Hospitali nyingi za umma zimejitahidi kutoa huduma mbalimbali za afya katika mazingira magumu mno ya kazi na baadhi zimekuwa sehemu ya kupoteza maisha

ya binadamu na/au kupata mateso badala ya tiba na kuwa kero isiyokoma kwa wagonjwa. Mamilioni ya vijana wa Kitanzania hawana ajira kwa sababu ya elimu duni waliyoipata. Tanzania imekuwa nchi ambayo mafanikio ya mtoto huko mbele yanategemea alizaliwa wapi na nani, badala ya kutegemea juhudi, bidii na fursa sawa.

Lakini matatizo haya yote na mengine hayakushushwa kutoka mbunguni, na wala sio kwamba yametokea kwa bahati mbaya. Kwa makusudi na mkakati, CCM wameiharibu nchi hii hatua kwa hatua, sisi sote tukiwaangalia na wakati mwingine tukiwashangilia. Tumekabidhi madaraka kwa kikundi kidogo cha watu ambao wamehodhi madaraka kwa makucha ya kisiasa, nguvu za kiuchumi na mfumo wa kijamii. Ni kikundi hiki ambacho kimeharibu juhudi zetu za kujipatia uhuru wa kweli, kujenga jamii inayoheshimu wajibu na fursa kwa wote.

Viongozi wa CCM wanaelekea kutuaminisha kwamba ufisadi, ubinafsi, uchoyo, uvivu, ubabaishaji, ujanjaujanja na kutokujali ndio njia ya maisha na ndio Utanzania mamboleo. Kosa kubwa tulilofanya ni kuendelea kuamini kwamba haohao walioharibu ndio haohao watakaotengeneza. Lazima tukikatae kikundi hicho kidogo na tuifukuze CCM madarakani kwa kupitia mapinduzi baridi, mapinduzi ya amani, mapinduzi katika sanduku la kura. Kama tunataka tuirudishe nchi yetu na utawala wake mikononi mwa wananchi na katika misingi sahihi ya kidemokrasia, ambayo kwa sasa CCM wameipoka.

Tunahitaji tuanze upya. Tukubali kwamba tumekosea njia kama Taifa, na Taifa linaundwa na sisi wananchi kwa sababu viongozi tunawaweka sisi wenyewe Wananchi. Huu ndio msingi wa ilani hii. Tunaamini kwamba tunahitaji kuanza katika msingi mpya: ***uzalendo, maadili na uadilifu.*** Hii ndio misingi asili ya utanzania.

Falsafa ya CHADEMA ni **nguvu ya uma**. Umma utapata nguvu tu iwapo kuna *uhuru wa kweli, usawa, wajibu na fursa kwa kila Mtanzania.* Haya yanawezekana iwapo pana uongozi wa ***kizalendo, adilifu, makini*** na ***wenye upeo***. Kwa kuzingatia misingi hii, CHADEMA imeweka vipaumbele tisa vifuatavyo katika ilani ya uchaguzi huu. Vipaumbele hivi ni:

1. Fursa kwa kila Mtanzania kupata ***elimu bora***
2. Fursa kwa kila Mtanzania kupata ***huduma bora za jamii***
3. Wajibu wa serikali kufanikisha ***Kilimo bora***
4. Fursa kwa kila Mtanzania kumiliki ***uchumi imara na shirikishi***
5. Wajibu na fursa kwa kila Mtanzania katika kupata ***uongozi bora na mfumo mpya wa utawala***
6. Fursa kwa kila Mtanzania kupata ***ajira na ujira bora***
7. Wajibu wa ***kuimarisha ulinzi na usalama kwa kuzingatia matishio ya kisasa na mbinu za kisasa.***
8. Wajibu na fursa ya ***kukuza nafasi ya Tanzania katika diplomasia ya kimataifa***
9. Wajibu na fursa ya ***kuinua na kukuza sanaa, michezo na utamaduni wa Mtanzania***

SURA YA PILI

2. FURSA KWA KILA MTOTO WA KITANZANIA KUPATA ELIMU BORA

2.1 Utangulizi

CHADEMA inaamini kuwa elimu ndio nguzo kuu ya maendeleo na nyenzo ya haraka na ya uhakika zaidi ya kujenga taifa la kisasa. Wananchi wasio na elimu au wenye elimu hafifu hawawezi kupata fursa za kumiliki na kuendesha uchumi, hawawezi kuiwajibisha serikali yao na hawawezi kuwajibika. Kwa hivyo kutoa fursa katika kupata elimu bora ni hatua ya kwanza na ya msingi katika kujenga taifa linalojitegemea na lenye uchumi imara na maendeleo endelevu.

2.2 Hali halisi kuhusu elimu hapa nchini

2.2.1 Kuna matatizo mawili ya msingi kuhusu elimu hapa nchini. Tatizo la kwanza ni uduni wa elimu inayotolewa katika shule zetu, na hasa shule za umma. Ukiwauliza CCM kuhusu elimu wanakujibu kuwa Taifa limepiga hatua kubwa ya upanuzi wa fursa za elimu hapa nchini, hasa elimu ya sekondari kufuatia kuanzishwa kwa Mpango wa Elimu ya Sekondari (MES). Hii ni kweli kwa upande mmoja. Mfano mzuri ni kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na shule za sekondari, hasa za kata, kutoka wanafunzi 345,441 mwaka 2003 hadi kufikia wanafunzi 1,466,402 mwaka 2009.

2.2.2 Hata hivyo, Serikali ya CCM iliahidi kupitia Mpango wa Elimu ya Sekondari (MES) kuongeza kiwango cha kufaulu katika madaraja ya I, II na III toka asilimia 37.8 mwaka 2004 hadi kufikia asilimia 70 mwaka 2009. Lakini, pamoja na kwamba Serikali ya CCM kwa msaada wa mashirika ya kimataifa imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 200 chini ya Mpango wa Elimu ya Sekondari, kiwango cha kufaulu katika madaraja haya kimeshuka. Kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu za Baraza la Mitihani la Taifa na Kijitabu cha Takwimu cha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, idadi ya wanafunzi wanaofaulu katika madaraja ya I, II na III kimeshuka kutoka asilimia 37.8 mwaka 2004 hadi asilimia 17.8 tu mwaka 2009. Aidha, idadi ya wanafunzi wanaofeli kwa kupata Daraja la 0 (Division 0)

imeongezeka kutoka asilimia 8.5 mwaka 2004 hadi kufikia asilimia 27.49 mwaka 2009. Asilimia 54.66 ya watahiniwa wote wa Kidato cha Nne mwaka 2007 walifaulu kwa kiwango cha Daraja la IV, ambalo kimsingi ni sawa na kufeli.

2.2.3 Chanzo kikubwa cha tatizo la uduni wa elimu yetu ni sera mbovu za elimu na uongozi legelege katika Wizara ya Elimu na Serikali ya CCM kwa ujumla. Sera za CCM kuhusu elimu ni bora elimu; kwao wingi wa mashule ndio elimu yenyewe bila kujali wanachokipata wahitimu wa mashule hiyo. Kwa miaka nenda wameendelea kutuhubiria juu ya *kuboresha* elimu huku wakitekeleza sera ya *kubabaisha* elimu Serikali ya CHADEMA itatilia mkazo ***elimu bora*** na hiki ndicho kitakachokuwa kipaumbele cha kwanza katika sera ya elimu.

2.2.4 Tatizo la pili la msingi linahusu mfumo wa elimu hapa nchini. Mfumo wetu wa elimu haumfanyi mhitimu aweze kujitegemea. Ni mfumo unaotaalumisha bila kutalaamisha. Hii inafanya vijana wanaohitimu masomo yao wasiweze kujitegemea kikamilifu nje ya mfumo rasmi wa ajira.

2.2.5 Pamoja na matatizo haya ya msingi, kuna matatizo sita mahususi katika elimu yetu ambayo CHADEMA itakabiliana nayo mara baada ya kuunda serikali.

i. Matabaka katika elimu na kutelekezwa kwa shule za umma

Serikali ya CCM imezitekeleza shule za umma. Shule nyingi za serikali zimechakaa kimajengo, hazina madawati, vitabu, maabara na vifaa muhimu vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia. Watoto wanaosoma katika shule za serikali wanasoma katika mazingira magumu sana. Kwenye shule kadha wa kadha za bweni na za kutwa lishe bado ni tatizo na ni duni. Matokeo yake wazazi wenye uwezo wanalazimika kuwapeleka watoto wao katika shule za binafsi, ambazo ni chache na ghali. Matokeo yake tumetengeneza ubaguzi katika mfumo wa elimu kati ya shule binafsi na za serikali. Hali hii ni hatari kwa mustakabali wa taifa kwa muda mrefu ujao.

ii. ***Kudhalilishwa kwa taaluma ya ualimu kiujira na kitaaluma:*** Walimu wa shule za serikali wametelekezwa kwa kulipwa mishara midogo na wanafanya kazi katika mazingira magumu na ya kudhalilishwa. Matokeo yake, walimu walio wengi

wamekata tamaa, na wakipata mwanya wa kazi nyingine huacha ualimu mara moja. Bado walimu ndio viongozi wa awali kabisa ambao watoto wetu wanakutana nao katika makuzi yao na ni kutoka kwao ndio wanajifunza tunu mbalimbali za maisha. Kutotengeneza mazingira na mfumo mzuri wenye kujali maisha na kazi ya ualimu ni kuweka msingi mbaya kwa wanafunzi wao kujifunza kutoka kwao na kuwaiga.

iii. ***Watoto wa kitanzania kutojengewa msingi mzuri wa lugha ya taifa na za kimataifa hasa Kiingereza***. Katika ukanda wa Afrika Mashariki (EAC) na Kusini mwa Afrika (SADC), ni watoto wa kitanzania pekee wasiofundishwa lugha ya kiingereza kwa ufasaha. Matokeo yake, ili mtoto ajifunze lugha kama ya Kiingereza vizuri ni lazima apelekwe kwenye shule binafsi za *international*. Wale wasio na nafasi hizo wanajikuta katika hali ngumu ya kujifunza katika ngazi za juu za elimu ambazo zinahitaji ufasaha mkubwa wa lugha ya Kiingereza kuweza kuelewa na kujieleza. Kumudu lugha hii si kwa ajili ya ajira tu bali kwa ajili ya kujenga uwezo wao kuhusiana na kushirikiana katika ngazi mbalimbali za maisha na watu wengine ambao lugha inayowaunganisha ni ya Kiingereza au Kifaransa.

iv. ***Utoro na Watoto wa kike kuacha shule kwa sababu ya mimba*** Moja ya tatizo linaloikabili elimu yetu ni utoro wa wanafunzi. Takwimu za elimu zinaonyesha kuwa utoro wa wanafunzi wa shule za msingi umefikia kiwango cha asilimia 35.5, na baadhi ya mikoa na wilaya hadi asilimia 56.7. Takwimu zinaonyesha pia kwamba mimba za utotoni ni moja ya sababu kubwa za watoto wa kike kuacha shule, ambapo asilimia zaidi ya 15 ya watoto wote walioacha shule mwaka 2009 ilisababishwa na mimba za utotoni.

Kinachoshangaza zaidi ni kwamba ***Rais Kikwete***, badala ya kuja na suluhu ya tatizo, ***anawalaumu watoto wanaopata mimba kwa kuwaambia kuwa wanapata mimba kwa sababu ya 'kiherehere chao'*** (Nipashe, Jumatatu, 07 Juni 2010). Tunahitaji ufumbuzi wa haraka na wa kudumu wa tatizo la watoto wetu wa kike kuacha shuke kwa sababu ya mimba.

Serikali ya CHADEMA itaweka utaratibu ili kuhakikisha kuwa wanafunzi ambao wanajikuta wanalazimika kukatisha masomo kwa sababu ya ujauzito wanaruhusiwa kuendelea na masomo mara baada ya kujifungua bila kulazimika kuhama maeneo yao kwa sababu ya unyanyapaa. Tanzania imepoteza mabinti wengi walioachishwa shule kwa sababu ya ujauzito ambao kama wangepata nafasi ya kuendelea na shule wangeweza kutoa mchango kwa taifa

Pamoja na hilo, Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa wale wote wanaowapatia wanafunzi mimba wanawajibishwa kisheria pamoja na kulazimishwa kulipia gharama yote ya kukatisha masomo na malezi ya mtoto hadi mtoto afikapo miaka 18. Na wale ambao wanafanya vitendo hivyo kwa mabinti wa chini ya miaka 18 watashtakiwa kwa mujibu wa sheria kwa makosa ya ubakaji (statutory rape).

v. ***Kufifishwa kwa shule za kitaifa*** Serikali ya CCM imeondoa shule za kitaifa ambazo zilikuwa ni muhimu katika kujenga moyo wa utaifa miongoni mwa vijana na wananchi kwa ujumla kwa kuwapokea wanafunzi kutoka sehemu kila pembe ya nchi. Matokeo yake kuna watoto wanaoanza shule katika kata na wilaya moja kuanzia shule ya awali hadi kidato cha sita na kuna baadhi wana hatari ya kusoma hadi chuo kikuu katika wilaya moja. Hii si hali nzuri kitaifa kwa sababu inawafanya vijana wawe na mawazo finyu na kutokutambua hali halisi ya nchi yao, na hivyo hubomoa mshikamano wa kitaifa.

vi. ***Mfumo usio wa uhakika wa kugharamia elimu ya juu.*** Serikali ya CCM imeshindwa kubuni njia endelevu za kugharamia elimu, na hasa elimu ya juu. Kukosekana kwa njia za uhakika za kugharamia elimu ya juu kumesabisha matatizo mengi katika sekta ya elimu ya juu ikiwemo:

    - Vyuo vikuu na taasisi nyingine za elimu ya juu kukabiliwa na uhaba mkubwa wa fedha kunakopelekea vishindwe kutimiza majukumu yao ya msingi kikamilifu. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, baadhi ya vyuo vikuu vilipata asilimia 30 tu ya bajeti ilivyopangiwa.

- Kushindwa kwa Serikali ya CCM kugharamia tafiti zinazofanywa katika vyuo vyetu, na tafiti chache zinazofanywa zinagharamiwa na wafadhili wa nje. Ni wazi kuwa tafiti za namna hii haziwezi kuwa na ajenda endelevu ya kujibu matatizo ya nchi kwani wanaofadhili tafiti wana ajenda zao ambazo wangependa zitimizwe

- Kushindwa kuwa na mfumo endelevu wa kufadhili au kuwapa mikopo wanafunzi katika vyuo vikuu. Mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu inatolewa kimatabaka, kwa usumbufu mkubwa, na mara nyingine wanapata wasiotahiki na wanaostahiki hawapati.

- Vyuo vikuu kupoteza uhuru kamili wa kufanya kazi za kitaaluma na kitaalamu kunakosababishwa na kuingiliwa na wanasiasa. Imefika mahala hata ajira za vyuo vikuu sasa hivi zinaamuliwa na wanasiasa badala ya mabaraza ya vyuo hivyo kwa kuzingatia sifa zao za kitaalma na kimaadili.

- Kasi ndogo ya maendeleo katika sekta ya sayansi na teknolojia kunakosababishwa na uwekezaji mdogo katika sekta hii na kutowajali wana sayansi kimaslahi, hasa walio katika sekta ya umma.

2.3 CHADEMA itafanya nini?

CHADEMA inaamini kuwa kuwekeza katika elimu ndio nyenzo kuu ya kukabiliana na matatizo yote yanayoikabili nchi yetu, ikiwemo umaskini. Tukifanikiwa kuwa na elimu bora tutakuwa tumejipatia silaha muhimu ya kukabiliana na maadui ujinga na maradhi na nyenzo muhimu ya kukuza uchumi imara na shirikishi. Hivyo basi, Serikali ya CHADEMA itatilia mkazo sana ubora wa elimu badala ya bora elimu.

Katika kuinua ubora wa elimu CHADEMA inaamini kuwa ***Elimu bora ni walimu bora.*** Hivyo basi, CHADEMA itaweka mkazo katika kuwapatia walimu mafunzo bora na ujira stahiki ili waweze kuwa na maarifa ya kutosha na kutulia mashuleni. Tutaweka mkazo katika kuwapatia watoto wa shule kiwango cha juu katika elimu kuanzia chekechea hadi chuo kikuu. Mkazo utawekwa katika kuhakikisha kuwa shule na taasisi zote za elimu zinatoa elimu inayochochea fikra, udadisi, maarifa na ugunduzi na inayoibua vipaji.

Lengo ni kuhakikisha kuwa kila hatua ya kielimu inamuwezesha mhitimu kujitegemea na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi na jamii aliyomo.

Katika kutekeleza haya, serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

2.3.1 Kuhusu Elimu ya Msingi na Sekondari

- Lengo la Serikali ya CHADEMA ni kubadili mfumo wa elimu ya msingi ili iweze kujitoshekeza kwa kuhakikisha kuwa wahitimu wanapata maarifa na stadi za maisha zitakazowawezesha kujitegemea kimaisha. Ili kufikia adhima hii, tutafanya mabadiliko yafuatayo:

    - Muda wa elimu ya msingi utaongezwa kutoka miaka saba (7) hadi miaka kumi. Hii inamaanisha kuwa watoto watamaliza shule wakiwa na umri wa miaka 16/17, umri unaomwezesha kuanza maisha ya kazi kwa mujibu wa sheria za nchi na kimataifa

    - Mtaala wa elimu ya msingi utapanuliwa kwa kuingiza muhtasari wa kidato cha kwanza na cha pili cha sasa kuwa sehemu ya elimu ya msingi

- Elimu ya Sekondari itabadilishwa kutoka miaka sita (6) hadi minne (4) kwa kuunganisha mihtasari ya kidato cha tatu,nne, tano na sita kuwa muhtasari mmoja wa elimu ya sekondari. Hii itasaidia sana kuongeza idadi ya wanafunzi wanaopata sifa za kujiunga na elimu ya sekondari.

- Kuimarisha shule za umma ili zitoe elimu bora. Hili litafanywa kwa kuanzisha kampeni ya kujenga upya, kukarabati na kuzipatia shule zote nchini huduma muhimu za jamii hasa maji safi na umeme.

- Kuhakikisha kuwa ndani ya miaka mitano ya utawala wa Serikali ya CHADEMA kila mtoto mwenye umri kati ya miaka 4 na 5 anahudhuria elimu ya awali kabla ya kuanza elimu ya msingi. Hii ni hatua muhimu kwa kuwa tafiti zinaonyesha kuwa watoto waliohudhuria elimu ya awali huanza shule ya msingi wakiwa na msingi bora zaidi kuliko wale ambao hawakupitia elimu hiyo.

- Kuimarisha ufundishaji wa Lugha ya Kiingereza. Hili litafanywa kwa kuboresha mazingira mazuri ya kujifunzia lugha ya Kiingereza, ikiwemo kuzipatia shule walimu wenye ujuzi wa kufundisha lugha ya Kiingereza. Lengo likiwa ni kuhakikisha mwanafunzi anapoingia kidato cha pili anafahamu lugha ya kiingereza katika kuelewa, kuandika, kusema na kujieleza.

- Kuimarisha ufundishwaji wa lugha ya Kiswahili. Pamoja na mkazo wa lugha ya Kiingereza, Serikali ya CHADEMA itaweka msisitizo wa pekee wa kuifahamu lugha ya Kiswahili pamoja na Kiingereza. Wanafunzi wa kitanzania ni lazima waimudu lugha yao ya taifa bila kujiona duni na wakati huo huo wakijiimarisha katika lugha ya Kiingereza.

- Kuimarisha ufundishaji wa Sayansi na Hisabati kwa kuandaa walimu wa masomo hayo kwa uhakika, kujenga maabara za masomo hayo zenye vifaa vyote vya msingi pamoja na kemikali vinavyohitajika. Kwa upande wa somo la elimu viumbe, shule zitaweka utaratibu wa kufuga wanyama wadogo wadogo na kutunza mimea ya aina mbalimbali kwa ajili ya kufundishia. Ufundishaji wa Hisabati utaboreshwa ili uendane na misingi yake ambayo inazingatia sayansi ya kimantiki inayojengeka hatua kwa hatua ili kuondokana na tatizo la kukaririshwa, na hivyo kuinua kiwango cha kufaulu katika somo hili.

- Kuinua ujira wa walimu kwa kuangalia upya viwango vyao vya mishahara na kuimarisha mazingira ya kazi na kimakazi. Katika kuboresha mishahara ya walimu, na wafanyakazi wengine wote katika sekta ya umma, tutaweka fomula ya kupandisha mishahara kwa kadri mfumuko wa bei na gharama za maisha zinavyopanda kwa kutumia mpango wa Scala Mobile, ambayo ndio inayotumika katika nchi nyingi duniani. Hii ndio kusema kila mara ambapo mfumuko wa bei utapanda na hivyo gharama za maisha kupanda, mshahara nao utapanda. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanamudu gharama za maisha ya kawaida ili waweze kuwekeza muda na utaalamu wao katika kulitumikia taifa. Utaratibu huu pia utaondoa umuhimu wa migongano baina ya Serikali na vyama vya wafanyakazi.

- Sambamba na kuboresha mishahara ya wafanyakazi kwa ujumla, Serikali ya CHADEMA itarudisha posho ya mazingira magumu kwa walimu wanaofundisha maeneo magumu ya vijijini hasa katika mikoa inayotambulika kuwa ni ya pembezoni.

- Kupitia upya mfumo na mtaala wa elimu ili:

    - Kuhakikisha kuwa, pamoja na taaluma, wahitimu wanapata utaalamu na stadi sahihi za kujitegemea. Serikali ya CHADEMA itabadili kabisa mfumo wa sasa wa elimu ili kutoa fursa kwa vijana walio wengi wapate utaalamu na stadi za kujitegemea mapema.

    - Kuhimiza ufundishwaji wa stadi za maisha na TEKINOHAMA kwa kuhakikisha kuwa matumizi ya teknolojia ya kisasa yanaanza mapema kwa wanafunzi wetu ili kuweza kuwaleta katika kiwango cha kimataifa cha elimu na ujuzi mapema inavyowezekana.

- Kuingiza katika mitaala elimu ya uzazi na mahusiano kuwiana na umri wa wanafunzi. Ufundishwaji wa somo hili litawapatia vijana wa kike stadi za kuweza kujikinga na tatizo la kuanza ngono katika umri mdogo. Nchi nyingi zilizofanikiwa kupunguza au kumaliza tatizo la mimba utotoni ni zile zinazozingatia utolewaji wa elimu ya uzazi na mahusiano mashuleni. Elimu hii itazingatia uelewa wa kisayansi kuhusu maisha ya watu, lakini vile vile utazingatia umuhimu wa kulinda familia na maamuzi ya wazazi juu ya watoto wao kwa kuhakikisha elimu inayotolewa ni ile yenye kuzingatia heshima, kujiamini na kujilinda katika mahusiano ya kijinsia.

- Elimu ya ngazi ya msingi na sekondari itagharamiwa na serikali kuu pamoja na serikali za mitaa. Lengo ni kuhakikisha kuwa elimu hii ya msingi kabisa inakuwa ni haki kwa kila mtoto wa Kitanzania na kiwango cha ubora kinalingana kwa nchi nzima.

- Ili kukabiliana na wimbi la utoro na usinziaji darasani kwa sababu ya njaa miongoni mwa watoto wa shule, Serikali ya CHADEMA itarudisha utaratibu wa kutoa chakula cha mchana mashuleni, ambayo kitagharamiwa na serikali za halmashauri za miji na

wilaya pamoja na serikali za mitaa na vijiji, kwani mtoto mwenye njaa au asiye na uhakika wa lishe hawezi kuzingatia elimu.

- Tutazihuisha na kuanzisha shule mpya za kitaifa za bweni za sekondari. Shule hizi zitachukua wanafunzi wote waliofanya vizuri zaidi katika mitihani yao ya mwisho ya elimu ya msingi. Katika kila mkoa kutakuwa na angalau shule moja ya kitaifa itakayochukua wanafunzi kutoka katika mikoa mingine kwa lengo la kujenga utaifa na uzalendo miongoni mwa wanafunzi, na CHADEMA itarejesha utaratibu wa usafiri wa "Warrant" kwa wanafunzi hao ili kuondoa makali ya gharama za nauli kwa wazazi. Ni wazi kuwa utaratibu huu ni ghali, lakini kuua utaifa ni ghali zaidi!

2.3.2 Kuhusu Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu

CHADEMA kina lengo la kubadilisha na kuboresha sekta ya elimu ya juu ili iweze kuwa ya kisasa zaidi na inayomuandaa msomi wa Tanzania kushiriki katika kutumia elimu yake kuiletea maendeleo Tanzania na vile vile kumpa nyenzo za kisasa za kielimu kuweza kumuandaa na maisha ya ulimwengu wa kisasa. Lengo ni kuhakikisha kuwa elimu ya juu inapatikana kwa kila kijana wa Kitanzania anayetaka elimu hiyo, ni ya kisasa, na inamuandaa msomi kurudisha katika jamii ujuzi alioupata chuoni.

Katika kupanua wigo na kuboresha elimu ya juu, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

- Serikali ya CHADEMA itaanzisha mfuko wa elimu uitwao "Uhuru Scholarship Fund" kwa ajili ya kugharamia masomo katika chuo kikuu cha umma kwa wanafunzi wanaofaulu katika kiwango cha Daraja la I na II. Huu hautakuwa mkopo kwa kijana yeyote ila atalipiwa Chuo kwa kadiri ya kwamba anaendelea kufikia viwango vya juu vya kitaaluma kwa mujibu wa taratibu kwa muda wote atakaokuwa chuoni.

- Kwa wanafunzi ambao watafaulu madaraja mengine (daraja la tatu na la nne) mfumo mpya wa kugharimia elimu ya juu utawekwa ili kuhakikisha kuwa gharama ya elimu ya juu haiwi kizuizi kwa kijana yeyote anayetaka elimu ya Chuo Kikuu. Katika

kutimiza adhima hii, Serikali ya CHADEMA itahakikisha kila mkoa unaanzisha mifuko ya elimu ya Juu kwa ajili ya vijana wake, taasisi za dini na watu binafsi watawekewa utaratibu wa kisheria ili waweze kuanzisha mifuko ya elimu hasa inayotoa fedha zisizo mikopo (grants) kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kwa kuzingatia vigezo mbalimbali.

- Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu itavunjwa kutokana na uendeshaji mbovu, mfumo wake mbovu wa kisheria, na uongozi ambao umeshindwa kufanya elimu ya juu ipatikane kwa kila kijana na ambayo kutokana na uongozi usiofaa imeshindwa kukusanya madeni toka kwa wakopaji. Uchunguzi huru utafanyika wa fedha zote zilizotumika hadi hivi sasa na kuangalia kama waliopewa dhamana hawakutumia nafasi zao kujinufaisha. Miezi sita baada ya uchunguzi kufanyika ripoti itawekwa hadharani na mapendekezo yake kuanza kufanyiwa kazi mara moja.

- Serikali ya CHADEMA itaunda chombo kipya cha utoaji na usimamizi wa mikopo ya elimu ya juu ambacho kitajulikana kama Mamlaka ya Taifa ya Kugharimia Elimu ya Juu (Tanzanian Higher Education Financing Authority - TAHEFA). Hiki ndicho kitakuwa ni chombo cha kifedha ambacho kitachukua majukumu yote ya Bodi ya Mikopo ya sasa chini ya muundo mpya na sheria mpya itakayoweka utaratibu mpya na wa kisasa kutoa mikopo ya elimu ya juu na kuhakikisha hakuna kijana wa Kitanzania anayetaka elimu ya juu ambaye ataikosa.

- Vyuo vikuu vitapewa fursa ya kujiendesha, kuanzia utawala hadi kitaaluma bila kuingiliwa na serikali. Vyuo vikuu vitakuwa na fursa kamili ya kuchagua viongozi wao bila kuingiliwa na serikali. Kazi kuu ya serikali itakuwa ni kutunga sera za jumla za kuendeleza na kulinda ubora wa elimu ya juu, kuhakikisha rasilimali muhimu zinapatikana lakini uendeshaji wa vyuo vikuu utaachwa mikononi mwa mabaraza ya vyuo vikuu.

- Serikali ya CHADEMA itarejesha na kuruhusu uwepo wa siasa katika vyuo vikuu vyote nchini kama shughuli ambazo ni nje ya masomo. Hii itasaidia kujenga uwanja wa demokrasia katika serikali za vyuo na vile vile itasaidia katika kuweka mazingira

ambapo wasomi wetu wanaanza kujifunza mbinu na utendaji wa kisiasa katika mazingira ya elimu ili waweze kujifunza kuishi pamoja, kupingana kwa hoja na kujua jinsi ya kuvumiliana katika mazingira ya tofauti mbalimbali za kiitikadi, imani, na mtazamo. Uamuzi wa kufanya hivi utachukuliwa ndani ya siku mia moja za kwanza za utawala wa serikali ya CHADEMA. Utawekwa utaratibu mzuri ili shughuli za kisiasa zisiingiliane na zile za kitaaluma.

- Ili kuchochea ubunifu na kuviweka vyuo vyetu vikuu katika Nyanja za kimataifa, Serikali ya CHADEMA itaanzisha ***Baraza la Taifa la Utafiti (National Research Council)*** ambalo pamoja na jukumu lake la kuratibu na kusimamia tafiti mbalimbali za kisayansi na teknolojia, kazi yake mojawapo itakuwa ni kutoa fedha kwa vyuo vikuu kwa njia ya kuvipatia uwezo vyuo hivyo kufanya tafiti mbalimbali ambazo matokeo yake yanakoleza matumizi ya sayansi na teknolojia nchini. Vile vile baraza hilo litasimamia mashindano ya changamoto za kisayansi ili kuchochea utafiti na ubunifu. Kila mwaka zawadi nono ya fedha taslimu itatolewa kwa Chuo Kikuu na wabunifu mbalimbali wa vitu ambavyo havijabuniwa sehemu nyingine duniani. Uundwaji wa baraza hili utaenda sambamba na uunganishwaji wa baadhi ya taasisi mbalimbali za utafiti nchini chini ya baraza hili moja huku zikiendelea kuwa huru kiutendaji, lakini zikiweza kushirikiana na kutegemeana katika kufanya utafiti na kusimamia matumizi ya tafiti hizo.

- Ili kuchochea kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia, Serikali ya CHADEMA itabadilisha vyuo viwili vya sasa ili viwe viwe vyuo vikuu vya Teknolojia. Vyuo hivyo ni Mbeya Instute of Science and Techonology ili kiwe Mbeya University of Science and Technology – MUST pamoja na Chuo cha Ufundi Tanga kuwa Chuo Kikuu Kishiri cha MUST.

- Pamoja na kutoa elimu ya Chuo Kikuu na Shahada, Serikali ya CHADEMA itaanzisha utaratibu wa kuwa na Vyuo Vya Kati vya Jumuiya ambavyo vitatoa elimu sawa na inayotolewa katika miaka miwili ya kwanza ya Chuo Kikuu. Lengo ni kuanza kutengeneza kundi la wasomi wa elimu ya kati ambao kutokana na sababu mbalimbali wasingeweza kupata elimu kamili ya chuo Kikuu. Vyuo hivi vya Jumuiya

(Community Colleges) vitakuwa ni kiunganisha kati ya elimu ya Sekondari na Elimu ya Vyuo Vikuu na vitakuwa na uwezo wa kutoa Shahada Shirikishi (Associate Degrees). Mwanafunzi anayemaliza vyuo hivyo akitaka baadaye anaweza kuendelea na Elimu ya Chuo Kikuu katika taaluma yake kwa kuendeleza pale alipoachia na siyo kuanza kama mwanafunzi wa mwaka wa kwanza. Baadhi ya vyuo mbalimbali vya jamii vilivyopo sasa vitapandishwa ngazi na kuwa Vyuo Vikuu vya Jumuiya.

- Serikali ya CHADEMA itafufua Huduma ya Maktaba kwa kuhakikisha kuwa kila Halmashauri ya Mji inakuwa na mfumo wa Huduma ya Maktaba. Maktaba hizi zitatakiwa kuwa ziwe kwenye bajeti zote za kwanza za Serikali ya CHADEMA na ufikapo mwaka wa pili asilimia 50 ya Halmashauri zote nchini ziwe zimekamilisha ujenzi wa Maktaba za kisasa. Utakapofika mwisho wa ngwe ya kwanza ya serikali ya CHADEMA, asilimia 100 ya Halmashauri zote ziwe na mtandao wa Huduma za kisasa za Maktaba. Viongozi wa kisiasa na jamii watahimizwa kuonesha mfano wa kupenda kujisomea ili kuchochea moyo wa kujisomea kwa vijana na watoto wetu. Ili kuonesha mfano na umuhimu wa kujisomea Rais Dr. Slaa atakuwa na utaratibu wa kusoma na watoto wetu katika mojawapo ya maktaba nchini mara kwa mara.

- Ili kurudisha mori wa utumishi miongoni mwa wahadhiri wa vyuo vikuu, Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa katika bajeti yake ya kwanza, madeni yote ya wanataaluma ya posho ya pango kwa wanaostahili yanalipwa na mpango wa kuboresha mafao ya uzeeni unatekelezwa kikamilifu. Tunataka wasomi wetu wasiwe na hofu ya maisha ya kila siku na wajikite kweli katika kutoa elimu, utafiti na ushauri wa kitaalam.

- Ili kuendelea kutumia utaalamu na uzoefu wa maprofesa hapa nchini katika kuwanoa vijana wetu vyuo vikuu, Serikali ya CHADEMA itajadiliana na wanataaluma pamoja na Mabaraza ya Chuo na Senate zao kuona uwezekano wa kuongeza umri wa kustaafu kwa maprofesa kamili kutoka miaka 60 70, maadamu chuo husika kitakuwa kimejiridhisha kuwa maprofesa husika bado ni wataaluma kikamilifu.

SURA YA TATU

3. FURSA KWA KILA MTANZANIA KUPATA HUDUMA BORA ZA JAMII

3.1 Utangulizi

CHADEMA inaamini kuwa huduma bora za jamii ndio msingi mkuu wa nguvu kazi katika taifa lolote. Hivyo basi, Serikali ya CHADEMA itaweka mkazo katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii kwa watu wote na kwa wananchi wote. Pamoja na kuboresha huduma zingine za jamii, Serikali ya CHADEMA itajikita katika kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata fursa ya kupata huduma stahiki za afya na maji safi na salama. Hali halisi ya huduma hizi na hatua zitakazochukuliwa na CHADEMA katika kuziboresha zinaanishwa hapa chini.

3.2 Afya

3.2.1 Hali halisi kuhusu huduma za afya hapa nchini

Tangu Mwalimu Nyerere aondoke madarakani mwaka 1985, serikali ya CCM imeongeza wingi wa majengo mbalimbali ya vituo vya afya. Hata hivyo, imeshindwa kusimamia utoaji bora wa huduma za afya zinatolewa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma. Kutokana na mfumo mbaya wa usimamizi wa sekta ya afya, misingi imara ya kuimarisha sekta ya afya iliyowekwa baada ya uhuru imevunjwa na kubomolewa. Kama ilivyo kwa sekta ya elimu, serikali ya CCM imetelekeza Hospitali na Zahanati nyingi za umma. Leo hii kwenda kutibiwa katika hospitali nyingi za serikali ni kama kucheza bahati nasibu. Kina mama wanajifungulia sakafuni, idadi ya watumishi wa kada za afya bado ipo chini, kunakodhihirishwa na upungufu mkubwa uliopo hasa vijijini ambako mpaka sasa umefikia asilimia 65%.

Serikali ya CCM wanasema kwamba itawachukua miaka 40 ili kuweza kumaliza tatizo la upungufu wa wataalamu hapa nchini. Ni kwa sababu ya kukosa umakini na utashi katika kuwekeza kikamilifu katika sekta ya afya, CCM wameshindwa kutekeleza ahadi walizojiwekea wenyewe. Kwa mfano, Serikali ya CCM iliahidi katika ilani ya uchaguzi wa mwaka 2005 kupunguza vifo vya akina mama kutoka vifo 278 katika akina mama 100,000 wanaojifungua hadi 132 kufikia mwaka 2010. Hata hivyo, siyo tu kwamba

wameshindwa kufikia malengo waliojiwekea, lakini pia, badala ya kupungua, vifo vya akina mama wajawazito vimeongezeka hadi kufikia 292 kufikia mwaka 2009!

Aidha, katika zaidi ya miaka 20 iliyopita, serikali ya CCM haijaweka mkazo katika kuzuia magonjwa. Hali hii imepelekea kuendelea kushamiri kwa magonjwa ya kuambukiza kama vile malaria, kifua kikuu, magonjwa ya njia ya hewa, kuhara, kuhara damu, kipindupindu, minyoo,nk. Uwepo wa magonjwa haya, hususani kipindupindu, ni aibu kubwa kwa taifa ambalo limejipatia uhuru zaidi ya miaka 50 iliyopita. Mbaya zaidi ugonjwa huu umeendelea kutokea katika Mji mkuu wa nchi mwaka baada ya mwaka. Hali hii kwa kiasi kikubwa inachangiwa na kuzorota kwa huduma za Afya ya Jamii kama vile udhibiti wa majitaka, taka ngumu na ukosefu wa Elimu sahihi ya Afya kwa jamii.

Vile vile uboreshaji wa afya unaenda sambamba na uimarishwaji wa huduma za utafiti ambazo ndizo zinajenga msingi bora na za kisasa za huduma za afya. Mpaka sasa, Serikali ya CCM haijatoa kipaumblele kinachofaa kwenye suala zima la utafiti katika sekta ya Afya. Hali hii imepelekea huduma nyingi kuendelea kutolewa kwa mazoea bila kuzingatia mabadiliko yaliyopo.

Aidha, ajali za barabarani zimeendelea kuua Watanzania wengi kila mwaka, na hakuna jitihada zinafanywa na serikali ya CCM katika kukabiliana nazo, zaidi ya kutoa salamu za rambirambi kila ajali hizo zinapotokea.

3.3 CHADEMA itafanya nini kuhusu afya?

Katika kuimarisha huduma za afya zinazotolewa na sekta ya umma, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

- Katika mwaka wa kwanza wa serikali ya CHADEMA mpango wa ujenzi wa Hospitali za Taifa za Watoto (National Children Hospitals) utaanza ili hatimaye kwenye nchi yetu tuweze kuwa na angalau hospitali kubwa zisizopongua tano na angalau mbili za rufaa ambazo zitakuwa mahsusi kwa ajili ya kuhudumia watoto katika ngazi za awali na rufaa. Hii itapunguza msongamano katika hospitali

mbalimbali nchini ambazo zinahudumia maelfu ya watoto kila siku. Mikoa ambayo itakuwa na Hospiali hizo kuu ni Arusha, Singida, Rukwa na Mara na Kigoma wakati Hospitali za Rufaa za watoto zitajengwa au kubadilisha zilizopo huko Pwani na Mwanza. Chadema itaangalia uwezekano wa kufanikisha hili kwa kushirikiana na taasisi binafsi na zile za kidini.

- Kuweka mkazo katika kuzuia magonjwa, hasa malaria, kifua kikuu na UKIMWI. Mkazo utawekwa katika kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa haya sambamba na uboreshaji wa huduma za tiba kwa kuhakikisha dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinapatikana kwa wakati na katika vituo vyote vya umma. Kwa kuwa ugonjwa wa Malaria unaongoza katika kusababisha vifo nchini, serikali ya CHADEMA itaweka mkazo katika kuhakikisha mazalia ya mbu yanadhibitiwa. Pamoja na kuwa matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa ni muhimu katika kupambana na ugonjwa wa malaria bado sio suluhisho endelevu kwa sababu mbu hakusubiri uingie kitandani ndipo akung'ate; anakuuma ukiwa mahali popote. Hivyo mkazo zaidi utakuwa katika kudhibiti mazalia ya mbu, upuliziaji wa dawa na vyandarua vilivyotiwa viuatilifu. Aidha, ili kulinda afya za akina mama wajawazito matumizi ya dawa kwa ajili ya kujikinga na malaria wakati wa ujauzito yatatiliwa mkazo sambamba na utoaji wa madini lishe kwa ajili ya kuongeza damu kwa akina mama hao kwani wengi wao hupoteza maisha kutokana na upungufu wa damu.

- Ili kuhakisha jamii ya kitanzania inaondokana na magonjwa makuu yanayosumbua kwa sasa, huduma za tiba kwa magonjwa hayo zitakuwa bure katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini. Magonjwa haya ni Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI. Aidha huduma kwa mama wajawazito, watoto (chini ya miaka mitano) na wazee (zaidi ya miaka 70) zitakuwa za bure kwa utaratibu ambao utawekwa. Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa huduma za tiba kwa magonjwa haya inapatikana masaa 24 na siku saba za wiki, badala ya utaratibu wa sasa wa kutokufungua huduma katika vituo vya afya na zahanati siku za mapumziko na mwisho wa wiki.

- Huduma ya bima ya afya itakuwa hitaji la lazima kwa kila Mtanzania, bila kujali kama ni mfanyakazi wa serikali au la. Ili kuwawezesha wananchi vijijini na wale

wasio na ajira katika mfumo rasmi, Serikali ya CHADEMA itaanzisha utaratibu wa bima ya afya ya jamii (Community Health Insurance Scheme) ambapo kila Halmashauri na Mamlaka za Miji zitatakiwa kuweka utaratibu wa kuwezesha wananchi wake kujipatia bima nafuu ya umma kwa malipo ya chini kuliko yale ya makampuni au taasisi binafsi na kuhakikisha kuwa kuanzia sasa hivi huduma ya dharura itapatikana kwa kila mwananchi katika hospitali yoyote nchini.

- Ili kuimarisha afya za wananchi, serikali ya CHADEMA itahamasisha kilimo cha chakula cha asili kinacholimwa kioganiki (organic farming) na tutahimiza wananchi kula chakula cha kutosha chenye mchanganyiko wa viini lishe unaofaa (balanced diet). Ili kutekeleza hili, tutaimarisha elimu ya lishe bora ndani ya jamii zetu kupitia vyuo vya maendeleo ya wananchi.

- Kwa vile tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 38 ya watoto wa chini ya umri wa miaka 5 wamedumaa hapa nchini na katika nchi zingine Kusini mwa Jangwa la Sahara, na kuwa hali yaweza kufikia hata asilimia 50 ya watoto basi tatizo hili la kudumaa (stunting) ni lazima lionekane ni tatizo la afya ya jamii. Hivyo basi, kampeni mpya ya chakula bora itaanza mara moja nchini kote mara tu Serikali ya CHADEMA itakapoingia madarakani.

- Kuimarisha vyuo vya kada za Afya (Madaktari, wauguzi, wafamasia, maafisa wa afya, fundi maabara, watunza kumbukumbu za afya, wataalamu wa radiolojia) kwa kuwapatia mahitaji muhimu kwa ajili ya kuvifanya vyuo hivi viweze kuandaa wataalamu wa afya wenye ujuzi na ubora zaidi.

- Kuongeza mishahara kwa watumishi wa sekta ya afya ili kuweza kuwavutia wataalamu kubakia nchini badala ya kwenda kutafuta kazi nje ya nchi kutokana na malipo mazuri huko. Wakati umefika kufanya kile ambacho tunakijua kuwa afya ni sehemu muhimu sana ya kujenga taifa la watu waliondelea.

- Kutoa posho ya mazingira magumu (Hardship allowance) kwa watumishi watakaokuwa sehemu ambazo ni ngumu kufikika huko vijijini pamoja na ujenzi wa

makazi ya maafisa wa afya katika maeneo hayo. Posho hizi zitatolewa katika mikoa ya pembezoni na hazitatozwa kodi.

- Kutenga fedha za kutosha kinachofikia asilimia kumi na tano (15%) ya bajeti ya wizara ya Afya kama ilivyo katika mikataba ya kimataifa.

- Kuimarisha mfumo wa huduma za afya mazingira kama vile uzoaji wa taka, majitaka na udhibiti wa uingizwaji wa vyakula vibovu toka nje. Aidha huduma za vyoo katika sehemu za umma zitapewa uzito wa kutosha. Ujenzi wa vyoo bora na vya kisasa utatiliwa mkazo ili kuondokana na vyoo ambavyo vimekuwa ni sehemu ya vyanzo vya magonjwa ya milipuko.

- Kuweka mfumo thabiti wa kudhibiti matukio ya ajali barabarani. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuhakikisha vyombo vya usafiri vinakuwa katika hali ya ubora unaotakiwa, kudhibiti utoaji holela wa leseni za udereva, kutoa adhabu kali (vifungo na faini) kwa madereva na wamiliki wa vyombo vitakavyosababisha ajali kwa uzembe. Aidha matumizi ya mikanda ya usalama kwenye magari ya abiria na binafsi litakuwa jambo la lazima. Vile vile hakuna chombo cha abiria ambacho kitaruhusiwa kubeba abiria zaidi ya uwezo wake.

- Kwa vile tatizo la watoto yatima limeongezeka sana kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo ugonjwa wa UKIMWI, Serikali ya CHADEMA itatunga sheria ambayo, pamoja na mambo mengine, itaweka utaratibu utakaosimamia kuchukua watoto wa kulea (adoption) na itasimamia vituo vya watoto yatima (orphanages) ili kuweza kuhakikisha kunakuwa na viwango vinakubalika vya kimataifa katika masuala ya malezi ya watoto yatima, na masuala ya kulea watoto yatima. Tutahakikisha kuwa sheria hiyo inakuwepo na inaanza kutekelezwa ndani ya miaka mitatu ya kwanza ya serikali yetu.

- Ili kukabiliana na upungufu mkubwa wa watumishi wa sekta ya afya hapa nchini, hasa madaktari, Serikali ya CHADEMA itapanua na kuendeleza maabara katika Vyuo Vikuu vyenye vitivo vya afya, na hasa Chuo Kikuu cha Afya cha Muhimbili.

Lengo ni kuongeza idadi ya madaktari na wataalamu wa afya na tiba mara tatu ya idadi iliyopo katika miaka mitano (5) ya awali ya Serikali ya CHADEMA.

3.4 Maji

CHADEMA inaamini kabisa kuwa maji ni uhai. Bila maji ya uhakika hapawezi kuwa na kilimo cha uhakika wala uzalishaji wa maana viwandani. Nchi isiyo kuwa na vyanzo vya uhakika vya maji salama na mfumo imara wa maji taka (sanitation) kwa wanaanchi wake ni nchi iliyojiweka tayari kukabiliwa na magonjwa maana magonjwa mengi chanzo chake ni maji yasiyo salama. Ndio kusema badala ya kusema Kilimo Kwanza, tunapaswa kusema Maji Kwanza, maana maji ndio msingi wa Kilimo Bora.

3.4.1 Hali halisi ya huduma za maji nchini

Pamoja na jitihada zilizofanyika katika kusambaza maji salama nchini, ni Watanzania asilimia 55-60 pekee wanaopata maji salama hapa nchini, wengi wao wakiwa mijini. Aidha, ni asilimia 24 pekee ya Watanzania wote ndio wanaotumia mfumo wa maji taka (sanitation). Uduni wa huduma za maji taka hapa nchini ndio hasa chanzo cha magonjwa ya kipindupindu ambacho hakiishi hapa nchini.

Aidha, ni chini ya asilimia moja (1%) ya wakuluma nchini ndio wanaotumia maji kwa ajili ya umwagiliaji mashambani. Kwa utaratibu huu itakuwa ngumu kufanikiwa kwa sera za kuendeleza kilimo, na kauli mbiu kama ‘Kilimo Kwanza’ zitaendelea kuwa nyimbo zisizo na tija.

Uwekezaji mkubwa wa kifedha uliofanyika katika sekta ya maji katika miaka ya karibuni umeshindwa kuleta tija kwa sababu ya ufisadi. Fedha nyingi zinazotolewa na wafadhili zinaishia kutafunwa na wajanja wachache katika CCM na serikali yake kupitia mikataba ya kitapeli, semina lukuki na posho zizoisha na zabuni hewa.

3.4.1 CHADEMA itafanya nini kuhusu maji?

Lengo la Serikali ya CHADEMA ni kuhakikisha kuwa Watanzania wanapata maji safi na salama na makazi ya watu yanaunganishwa katika mfumo wa maji taka. Vilevile, Serikali ya CHADEMA itatumia fursa za maji asilia kupitia maziwa na bahari katika kuinua na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Katika kutekeleza malengo haya, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

- Kuunda Wizara Maalumu ya Kudumu ya Maji ambayo itatengewa bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha sekta ya maji kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya na miji, ikiwemo kuhakikisha kuwa:
    - Wananchi angalau asilimia 60-70 wanapata maji safi na salama kufikia mwaka 2015. Kazi kubwa ya usambazaji wa mabomba ya kisasa ya maji itafanywa na halmashauri zote nchini ili kuhakikisha kiasi kikubwa zaidi cha maji kinawafikia wananchi kutoka vyanzo vyake na siyo kupotea kama inavyotokea sasa chini ya serikali ya CCM ambapo maji yamekuwa ni kama anasa ambayo watu hutumia muda mwingi kuitafuta na kuipata.
- Kuongeza idadi ya wananchi wanaotumia mfumo maji taka (sanitation) kutoka asilimia 33 ya sasa hadi asilimia 60 ifikapo mwaka 2015.
- Kutoa elimu kwa wananchi ikilenga katika kubadili tabia ili waweze kutunza vyanzo vya maji na kutunza mazingira kwa ujumla. Kuanzia vijijini hadi mijini jamii itasisitizwa kusimamia vyanzo vya maji na njia za maji ili kuona kuwa maji ni sehemu ya usalama wa taifa.

3.5 Uendelezaji makazi na nyumba

Chama cha Demokrasia na Maendeleo kitaandaa na kuanza kutekeleza mradi wa muda mrefu wa uendelezaji wa makazi na nyumba kwa Taifa zima ili hatimaye makazi na nyumba za wananchi wetu ziakisi maendeleo na mafanikio yanayotokea nchini. Katika

kutekeleza lengo hili, Serikali ya CHADEMA itavunja shirika la nyumba (NHC) kutokana na kushindwa kuleta mabadiliko ya makazi ya watu kama ilivyokusudiwa. Badala yake Serikali ya CHADEMA itaunda Mamlaka ya Taifa ya Uendelezaji Makazi na Nyumba (National Housing and Residence Development Authority) ambayo itakuwa na nguvu na muundo utakaowezesha kusimamia ujenzi katika makazi ya watu, miundombinu, na ubora wa makazi hayo ili yaendane na maisha ya kisasa ambayo Watanzania wanayatamani na kuyastahili. Chini ya Mamlaka hii kutakuwa na Ofisi ya Msajili wa Nyumba ambayo itamiliki na kusimamia nyumba mbalimbali za umma na ujenzi wa nyumba mbalimbali kwa ajili ya watumishi wa serikali.

<u>Mpango wa miaka kumi kuanzia 2010-2020 wa Uendelezaji Makazi ya Taifa (National Housing Development Plan) utalenga kuhakikisha kuwa:</u>

- Ujenzi wa nyumba za matope, fito na nyasi unatoweka nchini ifikapo mwaka 2020. Kiwango cha chini cha nyumba yoyote inayojengwa itakuwa ni nyumba ya matofali ya kuchoma na yenye kuezekwa bati. Hivyo, tutaandika sheria mpya ya ujenzi ili kuanza kukidhi mahitaji ya teknolojia ya kisasa pamoja na kufanya majengo yetu yawe ya kisasa kwa kila hali. Wakati wa kuondokena na nyumba za jadi kwenye makazi ya watu umefika. Hata wale watakaotaka kujenga nyumba zinazofanana na za jadi ni lazima watakiwe kufuata utaratibu mpya.

- Katika kutimiza adhama na lengo hilo serikali ya CHADEMA itaweka mfumo na utaratibu utakaosimamia na kufidia uvunjaji wa nyumba za zamani (ukiondoa zile ambazo zina umuhimu wa kihistoria, kidini, au uvunjaji wake utaingiliana na mipango mingine) na utafidia kwa kiasi gharama ya ujenzi mpya wa nyumba mpya ili kuhakikisha kuwa wamiliki wanarudi na kumiliki nyumba zao bila madeni makubwa migongoni mwao. Mpango huu hautabadili haki na hati za umiliki wa viwanja kwa wamiliki wake na wale wamiliki ambao hawakuwa na hati lakini wenye haki ya viwanja vyao watapatiwa hati hizo katika ujenzi huo mpya.

- Makazi yote ya watu yanafuata mifumo ya kisasa ya ujenzi ambayo inazingatia nafasi, usalama watu na afya. Lengo litakuwa ni kupanua mitaa, kuweka barabara za kisasa, na kupitisha na kufikisha huduma mbalimbali za kijamii.

- Kuanzisha mpango wa kuhakikisha kuwa maeneo yote ya makazi nchini yanapimwa, maeneo ambayo hayakupangwa kwa makazi yanahamishwa na maeneo mapya yaliyopangwa yanabuniwa. Lengo ni kuhakikisha kuwa Tanzania inajengwa katika maisha ya kisasa ambayo yanaonekana katika maeneo ya watu wanapoishi. Nyumba mpya za kisasa zitajengwa na mamlaka hii kwa ajili ya watu wa kipato cha chini na cha kati katika mfumo na mtindo wa kisasa wenye kuzingatia nafasi, usalama na afya na huduma muhimu za kijamii.

- Bajeti ya Serikali ya Taifa itatengwa ili kuhakikisha kuwa kati ya asilimia 8-10 ya bajeti yote ya serikali kila mwaka inatengwa kwa ajili ya kuendeleza makazi na nyumba.

3.6 Huduma kwa watu wenye ulemavu

Watu wenye ulemavu ni sehemu muhimu ya jamii yetu ambayo inahitaji sera maalumu za kulinda ustawi wao na kuwawezesha kutumia vipaji vyao katika kuchangia maendeleo ya nchi na ustawi wa jamii kwa ujumla. Inakadiriwa kuwa Tanzania ina watu wenye ulemavu wasiopungua milioni nne, ambayo ni takribani asilimia nne ya watu wote nchini.

3.6.1 Hali halisi ya huduma kwa watu wenye ulemavu nchini

Watu wenye ulemavu wanakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinaathiri moja kwa moja kiwango chao cha maisha na mchango wao katika maendeleo ya jamii. Baadhi ya changamoto na matatizo ya watu wenye ulemavu ni haya yafuatayo:

i) Ukweli kwamba huduma za jamii ni hafifu kwa ujumla wake katika nchi yetu ina maanisha kuwa ni hafifu na upatikanaji wake ni mgumu zaidi kwa wananchi wenye ulemavu. Bahati mbaya Serikali ya CCM haijaweka utaratibu wowote wa kuwawezesha watu wenye ulemavu kupata huduma za jamii kama vile afya na maji kufuatana na mazingira yao ya ulemavu

ii) Hakuna njia wala mkakati wa uhakika wa kutambua ulemavu mapema katika nchi yetu. Matokeo yake hatuna uwezo wa kuwatambua watu wenye ulemavu mapema ili kuweza kuchukua hatua za kuzuia na kutibu ulemavu pale panapostahiki. Hii ni pamoja na kushindwa kutambua watoto wenye mahitaji maalumu kabla hawajaanza shule ili kuweza kujiandaa kukidhi mahitaji yao. Walimu wengi wanashtukizwa na wanakuwa hawajui namna ya kuwasaidia watoto wenye ulemavu na mahitaji maalumu

iii) Kutokuwepo kwa vifaa maalumu vya kuwawezesha watoto wenye ulemavu kujifunza kikamilifu mashuleni.

iv) Watoto wengi wenye ulemavu hawapati fursa ya kwenda shule. Takwimi zinaonyesha kuwa ni chini ya asilimia moja (1%) tu ya watoto wenye ulemavu wanaopata fursa ya kujiunga na shule.

v) Matunzo duni na hali ngumu ya kimaisha inayowakabili watu wenye ulemavu kwa kuwa Serikali ya CCM haina mkakati wowote maalumu wa kuwasaidia.

3.6.2 CHADEMA itafanya nini?

Lengo kuu la sera ya CHADEMA kuhusu watu wenye ulemavu ni kuwawezesha watu wenye ulemavu kuishi maisha bora ili waweze kutoa mchango wao katika jamii kama walivyo Watanzania wengine. Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo katika kuboresha hali za maisha kwa watu wenye ulemavu.

- Kuhakikisha kuwa sheria ya kutobagua watu wenye ulemavu inaandikwa ili kuhakikisha kuwa Watanzania wote ambao wana ulemevau mbalimbali na bado wana uwezo wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa wanapewa nafasi hiyo bila ubaguzi wa aina yoyote ile kwa kadiri ya uwezo wao.

- Kuharakisha utekelezaji wa mfuko maalumu kwa ajili ya watu wenye ulemavu ambao utawawezesha kushiriki katika fursa za kiuchumi kwa njia ya mikopo.

- Kutoa mafunzo maalumu kuhusu stadi za maisha kwa watu wenye ulemavu kupitia vyuo vya VETA. Mafunzo haya yatagharamiwa moja kwa moja na serikali kupitia wizara husika

- Kutoa ajira za upendeleo kwa watu wenye ulemavu pale wanapokuwa na sifa zinazostahiki.

- Kuhakikisha kuwa kuna vifaa muhimu kwa mahitaji ya watu wenye ulemavu mashuleni na sehemu zingine za mafunzo. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa mashule na vyuo vyote vya umma vinahakikisha kuwa majengo yote yanaweza kuingilika na watu wenye ulemavu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa ngazi na njia zisizo na ngazi zinatengenezwa.

- Kuhakikisha kuwa majengo yote yanayojengwa yanazingatia na yale ya zamani yanaerekebishwa ili kukidhi mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa majengo hayo yote yanaingilika pasipo usumbufu kwa watu wenye ulemavu. Wizara na Taasisi za Serikali zitatakiwa kuwa za kwanza katika kutimiza adhma hii

- Majengo yote ya hadhara ambayo yana ghorofa yatatakiwa kisheria kuwa na lifti zinazofanya kazi kwa ajili ya matumizi ya watu mbalimbali wakiwemo walemavu.

- Kuhakikisha kuwa miundo mbinu yote muhimu ikiwemo barabara inatengenezwa na kurekebishwa ili kukidhi na kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

- Kuelimisha na kuhamasisha jamii ili kutambua na kuzingatia haki na mahitaji ya watu wenye ulemavu. Tutaweka makali katika sheria ili vitendo vyovyote vya dhulma, udhalilishaji, uovu na unyanyasaji kwa watu wenye ulemavu vinaadhibiwa mara moja na kwa ukali. Tunataka kurudisha tunu yetu ya Taifa iliyoasisiwa na Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere kuwa ***“kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake”.***

- Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa watu wote wenye ulemavu ambao kutokana nao hawawezi kabisa kujipatia kipato wanaishi kwa gharama ya umma. Katika kutimiza hili, tutahakikisha kuwa familia zenye walemavu wa aina zote zinapatiwa huduma mbalimbali za afya bure na kwa kushirikiana na vyama mbalimbali vya walemavu serikali itaandika upya sera ya walemavu ili kuhakikisha kuwa hakuna Mtanzania yeyote mwenye ulemavu anayekosa huduma ya afya, elimu, ajira, chakula au makazi.

SURA YA NNE

4. KUJENGA KILIMO BORA NA CHA KISASA

4.1 Utangulizi na hali halisi ya kilimo hapa nchini

Kilimo kinaendelea kuwa ndio chanzo cha kipato na ajira kwa Watanzania walio wengi. Aidha, kilimo ndio sekta inayochangia zaidi pato la taifa. Kwa hivyo ni muhimu kwa serikali yeyote iliyo makini kuwekeza katika kilimo kwa ajili ya ustawi wa jamii na maendeleo ya wananchi. Hata hivyo, Serikali ya CCM imeendelea kuchezea kilimo na wakulima kwa maneno matamu yasiyozaa tija. Kwa mfano, kwa muda mrefu waliimba wimbo kwa ‘Siasa ni Kilimo’, ’Kilimo cha Kufa na Kupona’, na sasa wameibuka na kauli mbinu ya ‘Kilimo Kwanza’. Bahati mbaya kauli hizi zimebaki kuwa kauli zisizoleta neema yeyote kwa wakulima. Hata juhudi nzuri zilizoanzishwa na Serikali ya Mwalimu Nyerere baada ya Uhuru zimebomolewa.

Kutokana na kutokuwa na mipango thabiti na ya muda mrefu ya kukuza na kuendeleza sekta ya kilimo, sekta hii imeendelea kukabiliwa na changamoto nyingi, ikiwemo:

- Nyenzo duni za kilimo kunakosababisha sekta hii isiwe na tija ya kutosha kwa wakulima walio wengi

- Sambamba na uduni wa nyenzo za kulimia, kilimo kimeendelea kutegemea mvua ambazo sio za uhakika kwa maeneo mengi ya nchi

- Kushindwa kuunganisha kilimo na sekta zingine za kiuchumi kama vile miundo mbinu, nishati, maji, viwanda na masoko

- Kutokuwa na masoko ya uhakika kwa mazao ya wakulima, hivyo kufanya kilimo kuwa ni kwa ajili ya chakula kuliko biashara. Kwa umbumbu wa maono au kwa makusudi Serikali ya CCM imewazuia wakulima kuuza mazao yao nje ya maeneo na nje ya nchi. Hii si tu kuwa ni dharau na matusi kwa wakulima, lakini ni unyanyasaji. Kudhani kuwa wakulima wakiruhusiwa kuuza mazao nje ya nchi itasababisha njaa ni dharau, umbumbu wa maono na kuwafanya wakulima kuwa

ni watoto wadogo wasioona mbali. CHADEMA inaamini kuwa wakulima wana akili na wanajua wauze chakula kiasi gani na kiasi gani wabakishe kwa ajili ya familia zao.

- Serikali kujitoa kabisa katika kusimamia shughuli za kilimo baada ya kuua vyama vya ushirika. Kujitoa kwa serikali katika kusimamia kilimo kumesababisha kilimo kiwe cha holela, kisicho na tija na ambacho hakichangii kikamilifu katika kuboresha maisha ya Watanzania. Na zaidi ya yote, Taifa limeendelea kukabiliwa na njaa kila mwaka. Hii ni aibu kwa nchi ambayo imejaliwa ardhi tele yenye rutuba na wananchi wenye nguvu na bidii ya kazi

4.1.1 CHADEMA itafanya nini kuboresha kilimo?

CHADEMA inaamini katika kilimo bora cha kisasa, na kuwa kilimo kwa sasa na muda mrefu ujao ndio nguzo kuu ya uchumi kwa Tanzania. CHADEMA inaamini pia kwamba ili kilimo kiweze kukua kinavyostahili na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi, ni muhimu kiwe na uhusiano na sekta zingine muhimu, zikiwemo mifugo, miundo mbinu, nishati na maji.

Lengo la CHADEMA kuhusu kilimo ni kuhakikisha nchi inakuwa na mazao ya kutosha kwa ajili ya mahitaji ya chakula na biashara. Ili lengo hili liweze kufikiwa, CHADEMA inaamini kwamba serikali lazima iwe na usimamizi mzuri na imara katika sekta ya kilimo. Aidha, CHADEMA inaamini kuwa ni makosa na ukosefu wa umakini na uzalendo kwa serikali kuachia kilimo mikononi mwa watu binafsi bila uratibu na usimamizi imara.

Serikali ya CHADEMA inalenga katika kuhakikisha kuwa kilimo cha Tanzania kinakidhi mahitaji makubwa mawili. Kwanza, kuweza kuzalisha mazao ya chakula kwa njia ya kisasa zaidi, kwa haraka zaidi na kwa kutumia muda mfupi na raslimali zetu kwa umakini zaidi ili kuhakikisha kuwa tatizo la njaa, utapiamlo na udumavu wa watoto unaondolewa. Tanzania ni lazima ijitosheleze katika mahitaji yake ya chakula kutokana na vyanzo vyake vya ndani. Pili, kilimo cha Tanzania ni lazima kiweze kuzalisha mazao ya chakula

na biashara ili kuweza kuwa chanzo cha kipato cha uhakika kwa wakulima wetu ili waweze kuinua maisha yao. Kilimo chini ya CHADEMA kitakuwa kweli ni cha kisasa na cha kumpatia mtu kipato cha kumfanya amudu maisha ya kisasa na kuweka akiba.

Hivyo basi, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo katika kujenga kilimo bora na cha kisasa:

- Tutahimiza matumizi ya mbolea ya asili za samadi na mboji katika maeneo ambayo mazao yanastawi kwa matumizi ya asili ya ardhi

- Kuanzisha ushirikiano na taasisi za kimataifa za kilimo cha kioganiki. Maeneo ya Lushoto, Tukuyu, Ileje, Mtwara, Lindi, Manyara, Kigoma, Singida na Tabora yatatengwa maalumu ili kuwe na sehemu ambazo zitatumika kuanzisha kilimo kikubwa cha kioganiki.

- Shule za Sekondari za Kilimo zitatumika katika kutoa mafunzo ya kilimo cha oganiki kama sehemu ya kuwaandaa wanafunzi katika maisha ya kilimo cha kisasa.

- Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine Morogoro kitatakiwa kuandaa mtaala ambao utaingiza mafunzo ya kilimo cha oganiki na kufanya utafiti katika mazingira ya Tanzania. Ushirikiano wa pekee katika hili utafanywa na taasisi mbalimbali za kilimo nchini ikiwemo Taasisi ya Kilimo ya Uyole ambayo itaanzisha utafiti wa mbegu mbalimbali za asili ambazo zinaweza kuotezwa bila kutumia madawa mengi ya viwandani au mbolea za viwandani.

- Pamoja na uwekezaji katika utafiti wa kilimo, tutahakikisha tunatafuta masoko ya uhakika ya mazao hayo ya kioganiki ambayo tunaamini yatakuwa ni ya ushindani mkubwa hasa huko Marekani, Canada, Ulaya na Mashariki ya Kati. Tunaamini kabisa kuwa mazao ya oganiki kutoka Tanzania yanaweza kuzalishwa kwa gharama nafuu kabisa kulinganisha na mazao hayo sehemu yoyote duniani na hivyo kulazimisha masoko hayo ya kimataifa kukimbilia Tanzania. Mtindo huu ndio umetumika katika nchi za Uchina na Uhindi katika kuvutia mataifa

mbalimbali kutafuta huduma na bidhaa kutoka huko. Katika kilimo Tanzania ina faida kubwa ya kiushindani (comperative advantage) kuliko nchi hizo na ni wakati wa kutumia faida hiyo kuinua kilimo chetu na maisha ya wakulima wetu.

- Kutilia mkazo kilimo cha mazao ambayo yana bei nzuri katika masoko ya ndani na ya kimataifa na gharama zake za uzalishaji ni nafuu. Mazao haya ni pamoja na nafaka mbalimbali kama vile karanga, alizeti, ufuta, kunde, dengu, choroko, mbaazi, n.k. Aidha tutahimiza kilimo cha mazao vikolezi na viungo kama vile pilipili, tangawizi, vitunguu swaumu, bilinganya, n.k. Katika kutekeleza hili, tutachukua hatua mahsusi zifuatazo:

- Zao la Mpunga ni miongoni mwa mazao ambayo yanaweza kabisa kubadilisha sehemu kubwa ya kilimo chetu. Hivyo maeneo kadhaa nchini yatapata upendeleo wa kimpango ili yaweze kuzalisha mpunga wa kutosha kwa mahitaji ya ndani na ya nje. Ili kutimiza hili, Serikali ya CHADEMA itatenga fungu la fedha maalumu baada ya kufanya uchambuzi yakinifu kila mwaka mahsusi kwa ajili ya kuhamasisha na kuendelza kilimo, utunzaji wa rekodi na uhifadhi wa mpunga na mchele. Serikali ya CHADEMA kupitia wizara na idara husika itatangaza tenda kwa wakulima wanaopenda kutekeleza mpango huu kuanzia bajeti yetu ya kwamza ya 2011/2012. Wakulima watakaoshinda tenda watapatiwa masharti na malengo maalumu yenye kulenga kufanikisha uvunaji wa kutosha wa mpunga kwa ajili ya chakula na kuuza nje. Kwa utaratibu huu tutaifanya Tanzania ijitosheleze kichakula wakati wote na iwe ndiyo msambazaji mkuu wa chakula cha mchele katika ukanda wa Afrika na mashariki ya mbali. Lengo la CHADEMA ni kuona kuwa Tanzania inajitegemea kwa chakula na kuanza kusafirisha nje mchele ndani ya miaka mitatu tangu iingie madarakani.

Mipango mingine ya kuboresha kilimo nchini itaangaliwa kiutalamu na uwekezaji wowote mkubwa katika kilimo nchini ni lazima uzingatie mahitaji ya chakula ya nchi. Katika hili:

- Serikali ya CHADEMA itapitia mikataba yote mikubwa ya kilimo ambayo imeingia na taasisi au nchi za nje ili kuweza kuhakikisha kuwa maslahi ya nchi na mahitaji ya chakula yanazingatiwa. Hii itakuwa ni pamoja na kuipitia mikataba hiyo na kuitengua ambayo itaonekana inahatarisha usalama wa chakula nchini.

- Serikali ya CHADEMA itaweka mkazo wa kukuza mazao mbalimbali ya nafaka kama ngano na shayiri kwa kuweka utaratibu utakayofufua mashamba makubwa ya mazao hayo nchini.

- Taasisi za nje au mataifa ya nje yanayotaka kuweza katika kilimo nchini yatatakiwa kufanya hivyo kwa kuingia mikataba na vijiji na maeneo husika ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi katika maeneo husika wanafaidika na uwekezaji mkubwa wa kilimo.

- Serikali ya CHADEMA itaweka msukumo wa kipekee kwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na vyuo vingine ili viwe ni vituo vya utafiti kwa vitendo katika mazao, mifugo na chimbuko la mbegu bora za nafaka. Lengo ni kuhakikisha kuwa nchi inajitosheleza katika mahitaji ya mbegu na kuliondolea taifa aibu ya kuagiz mbegu bora za nafaka kutoka nje ya nchi.

- Serikali ya CHADEMA itaangalia uwezekano wa kuanzisha kilimo cha mijini (urban farming) hasa katika mazao ya bustani za mboga na matunda. Lengo ni kuhakikisha kuwa katika miji yote mazao kama mboga na matunda yanapatikana kwa urahisi, katika mazingira safi na salama. Hii itakuwa ni pamoja na kuweka mfumo wa kuanzisha viwanda vidogovidogo vya kuhifadhia matunda na mboga. Uwekezaji mkubwa wa uhifadhi wa matunda na mboga utawekewa utaratibu hasa katika Mkoa wa Tanga kwa kuweka unafuu wa kodi kwa makampuni yatakayoanzisha viwanda vya kusindika matunda na mboga mkoano humo.

4.1.2 Mipango Mingine Kuhusu Kilimo na Mifugo

- Kuhimiza ufugaji bora ili mfugaji aweze kupata faida kutokana na ufugaji wake. Ili wafugaji waweze kuwa na nguvu katika kuuza mazao yatokanayo na ufugaji, tutahimiza uanzishwaji wa ushirika wa masoko (marketing cooperatives).

- Ili kukuza soko la mazao ya wakulima, vyama ushirika vitawezeshwa kushughulikia usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo, pamoja na bei na masoko ya mazao ya wana ushirika.

- Tutawekeza katika kutengeneza barabara zinaunganisha kata na kata, wilaya na wilaya na mikoa na mikoa ili kurahisha usafirishaji wa mazao kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

- Tutawekeza katika kupanua upatikanaji wa nishati ya umeme na maji vijijini ili kuweza kuchochea teknolojia ya kilimo

- Tutawekeza katika teknolojia ya kuvuna maji ya mvua, mabwawa, mito na maziwa ili kukuza kilimo cha umwagiliaji

- Ili kutekelezaji mipango ya kilimo ya muda mrefu, Serikali ya CHADEMA itaunda mamlaka inayojitegemea kwa ajili ya Kilimo (**Tanzania Agricultural Authority**). Kazi ya mamlaka haya itakuwa ni kuwekeza katika kilimo na kuhakikisha kuwa serikali inasimamia sekta ya kilimo kikamilifu, ikiwemo kuhakikisha kuwa wakulima wanakuwa na soko la mazao ya uhakika na kwa bei stahiki.

- Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa NARCO – Shirika la Ranchi la Taifa linaingia kwenye ushindani wa kibiashara katika uzalishaji wa nyama za chakula nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa pamoja na kuzalisha nyama kutoka mifugo ya kisasa, shirika hili linatumika katika kupata nyama za kioganiki (organic meat) yaani nyama ambazo wanyama wake hawakukuzwa kwa kutumia madawa ya viwandani.

- Ranchi zote za taifa zitapatiwa uwezo wa kibajeti ili ziweze kujiendesha kisasa ikiwemo kuzipatia vyombo vya kisasa vya mawasiliano ikiwemo utunzaji wa kumbukumbu za kompyuta na kuziunganisha ranchi hizo zote kwa mtandao wa kiintaneti.

- Mradi wa kuunganisha taasisi zote za utafiti wa kilimo na mifugo nchini kwa kutumia intaneti utatekelezwa ili ifikapo 2013 taasisi zote hizo ziwe katika mtandao wa kisasa wa mawasiliano.

- Ili kuhakikisha nyama za kioganiki ni za kisasa, taasisi mbalimbali za mifugo zitapewa uwezo wa kufanya tafiti za kupata wanyama bora wa kiasili (natural breeds). Jukumu hili litaingizwa kisheria na kuwa jukumu mojawapo la Taasisi ya Utafiti wa Mifugo ya Taifa (TALIRO) kuanzia katika bajeti ya 2011/2012.

- Kuweka utaratibu katika huduma na utendaji wa taasisi zote za umma kujipatia vyakula vyake vyote ndani ya nchi. Hii ina maana kuanzia siku serikali ya CHADEMA inaingia madarakani taasisi zote za umma zitatakiwa kufanya manunuzi ya mahitaji yake ya chakula kutoka katika vyanzo vya ndani. Hii itachochea ushindani, ubora na kuinua kilimo na mifugo ya ndani kwani soko la ndani kwa kiasi kikubwa litakuwa na uhakika. Hakuna ulazima kwa taasisi ya umma kununua mchele au vitunguu kutoka nje ya nchi. Uamuzi huu hautaingilia matumizi binafsi ya watu au taasisi binafsi.

- Kuwekeza katika uvuvi endelevu katika Bahari ya Hindi, maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ili kuongeza maradufu upatikanaji wa kitoweo kwa bei nafuu kwa wananchi walio wengi. Aidha, Serikali ya CHADEMA itashirikiana na nchi za Nordic, Korea ya Kusini na Japan ili kupata utaalam wa kilimo cha samaki baharini kwa mauzo ya nje.

SURA YA TANO

5. FURSA KWA KILA MTANZANIA KUJENGA NA KUMILIKI UCHUMI IMARA NA SHIRIKISHI

5.1 Utangulizi

Kutokuwa na ukuaji wa uchumi endelevu ndio chanzo kikuu cha utegemezi na umaskini wa nchi yetu. Hii inatokana na kushindwa kuvuna na/au kutumia raslimali za taifa kwa ajili ya manufaa ya nchi na wananchi wake, kunakosababishwa na kukosekana umakini, uzalendo na uadilifu miongoni mwa viongozi wa nchi. Kwa kifupi, uchumi wetu umeendelea kudorora kwa sababu ya uroho na vitendo vya kifisadi vinaendekezwa na watawala kwa kushirikiana na makampuni ya kigeni. Kwa hiyo, hatua yeyote ya kukuza na kuimarisha uchumi lazima ihakikishe kuwa inakomesha vitendo vya kifisadi katika usimamizi wa raslimali za taifa.

Lengo kuu la CHADEMA kuhusu uchumi ni kujenga uchumi imara na shirikishi, ili hatimaye mafanikio yeyote ya uchumi ya kitakwimu yaendane na kuboreka kwa hali za wananchi kunakoambatana na kupungua kwa gharama za maisha. Hivyo basi, Serikali ya CHADEMA itatilia mkazo katika kukuza uzalishaji kwenye uchumi mdogo (micro-economy) kama msingi wa ukuaji wa uchumi mkubwa (macro economy) ili kuhakikisha kuwa tunajenga taifa la wazalishaji badala ya taifa la wachuuzi tu. Ili kufikia malengo haya, tunahitaji serikali makini sana, imara na bora zaidi na yenye uadilifu na upeo mkubwa katika kipindi hiki cha utandawazi, inayoweza kusimamia uchumi na rasilimali zetu, la sivyo Watanzania wataendelea kuwa watazamaji na sio washiriki wa uchumi na raslimali zao.

Pamoja na kwamba kumekuwepo na ukuaji wa uchumi hapa nchini katika miaka ya karibuni, hasa kipindi cha serikali ya awamu ya tatu , ukuaji huu haujawa na manufaa kwa mwananchi wa kawaida, kwani umasikini umeendelea kuongezeka kila uchao.

Vile vile, kile kinachoitwa kuwa ni “ukuaji wa uchumi” ambao serikali ya CCM imekuwa ikiimba mara kwa mara ukiangaliwa kwa ukaribu utaonekana kuwa ni wa geresha, kwani siyo ukuaji wa uchumi bali ukuaji wa akaunti za watu wachache walio

katika madaraka. Watu hawa ndio wametumia nafasi zao mbalimbali na washirika wao kukuza “uchumi wao”.

Hii ni kwa sababu Serikali ya CCM imeshindwa kusimamia vilivyo shughuli za kiuchumi na kuhakikisha zinashirikisha wananchi. Badala yake, shughuli za kiuchumi zimekabidhiwa kwa vikundi vya watu wachache, wengi wao wakiwa ni wenye makampuni ya nje ambayo hayana maslahi ya moja kwa moja na nchi hii. Serikali ya CHADEMA itajikita katika kujenga uchumi imara unaowashirikisha wananchi kikamilifu, kwani bila uma kuhodhi uchumi na raslimali za nchi yao, CHADEMA inaamini kwamba haitakuwa rahisi kupunguza na kutokomeza umasikini mkubwa unaotukabili.

5.2 Hali halisi kuhusu uchumi wetu

5.2.1 Matatizo yetu ya uchumi yapo katika maeneo makuu sita yafuatayo:

- Kwanza kabisa ni matumizi mabaya ya fedha za serikali, kunakosababishwa na viongozi wa kisiasa na wale wenye dhamana katika taasisi za serikali kukosa uzalendo, umakini na uadilifu. Pengine tatizo kubwa zaidi katika miaka kumi iliyopita ni ufisadi, ambao uliasisiwa katika awamu ya tatu na kushamirishwa kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya katika awamu ya nne. Ukubwa wa serikali, matumizi ya anasa, ubadhirifu na ufisadi unaigharimu serikali fedha nyingi ambazo zingeelekezwa kwenye maendeleo ya nchi na utoaji wa huduma za kijamii.

- Tatizo la pili, ni serikali ya CCM kushindwa kubuni vyanzo vya mapato na hata kushindwa kusimamia ukusanyaji kodi kikamilifu. Kuna mianya mingi ya kukwepa kulipa kodi, hasa makampuni ya nje. Kwa sababu hii Waziri wa Fedha kila mwaka ameendelea kuongeza kodi katika vyanzo vilevile, kama vile pombe na sigara. Hii ni kama kuendelea kumkamua ng’ombe ambaye hanyonyeshi tena.

- Tatu, kutokana na matatizo yaliyotajwa hapo juu, serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kuliko uwezo wake wa kukusanya mapato ya ndani. Hii imeilazimu kutegemea misaada kutoka kwa wafadhili, jambo ambalo linaendelea kudhalilisha uhuru na azima yetu ya kujitegemea kama taifa. Tanzania imegeuka taifa omba omba na hotubu nyingi za Rais zimekuwa ni za kusifia na kupongeza misaada na wahisani, badala ya nini tufanye kama taifa.

- Nne, Serikali ya CCM kwa kuua viwanda tulivyoanzisha mara baada ya uhuru, na hasa baada ya kutangazwa Azimio la Arusha, kumetupelekea sisi kuwa nchi ya watumiaji na wachuuzi wa bidhaa tusizozalisha. Kwa sababu hiyo, kwa miaka 50 iliyopita Tanzania imeshindwa kufanya mabadiliko ya msingi na muhimu sana ya kiuchumi, toka kwenye kilimo cha kuhamia (subsistence agriculture) kwenda kwenya kilimo cha kisasa na kibiashara (mechanised and commercialized agriculture) kama hatua ya mwanzo ya kuelekea kwenya uchumi wa kisasa (manufacturing and services economy) wenye fursa nyingi za ajira na kipato kikubwa. Nchi yetu kwa miaka yote imebakia kuwa wasafirisha nje wa mali ghafi zenye tija ndogo sana badala ya bidhaa zilizozalishwa (i.e. processing and agri-business and manufacturing goods). Kutokana na udhaifu wa uchumi wetu, hali ya maisha ya wananchi wa kawaida imeendelea kuwa ngumu. Ajira zimekuwa chache na gharama za maisha zimepanda kwa kasi kubwa.

- Tano, uchumi wetu ni dhaifu kutokana na maendeleo dhaifu ya vichochea muhimu vya ukuaji wa uchumi, ikiwemo nishati na kushindwa kutumia vizuri raslimali asilia ambazo nchi yetu imejaliwa kama inavyoelezwa hapa chini.

- Sita, miundo mbinu, ambayo ndio kichocheo kikuu cha uchumi wa taifa lolote lile, hasa barabara, reli na bandari ni hafifu. Zaidi ya hapo tumeshindwa kutumia vizuri bandari zetu kutokana na ufanisi mdogo na vitendo vya kifisadi vinavyofanywa na viongozi wa Serikali ya CCM.

5.3 Nishati

5.3.1 Hali halisi ya nishati nchini

Sekta ya nishati nchini inakabiliwa na changamoto kubwa tatu. Changamoto ya kwanza ni kushindwa kupanuka kwa wigo wa vyanzo vya nishati hii zaidi ya kuendelea kutegema nishati ya kuni na mkaa. Vyanzo vikuu vya nishati nchini ni mkaa, ambapo zaidi ya asilimia tisini (90%) ya wakazi wanategemea mkaa na kuni kama ndio chanzo cha nishati, wengi wao wakiwa vijijini.

Changamoto ya pili ni idadi ndogo ya watu wanaotumia nishati ya umeme. Ni chini ya asilimia kumi na tano (15%) ya watu wote ndio waliounganishwa kwenye gridi ya taifa, na vijiji ni asilimia moja (1%) pekee ya wakazi ndio waliounganishwa katika gridi ya taifa.

Changamoto ya tatu ni Serikali ya CCM kushindwa kuoanisha ukuaji wa sekta ya nishati na ukuaji wa uchumi na idadi ya watu. Kwa sababu hii Serikali ya CCM imeshindwa kuwekeza vya kutosha katika sekta ya nishati kwa sababu inaona kama sekta hii ni anasa zaidi kuliko maendeleo. Nishati na miundo mbinu bora ndio damu ya ukuaaji wa uchumi wa taifa lolote lile duniani.

CHADEMA inaamini kuwa upatikanaji wa uhakika wa nishati ya umeme ni nyenzo muhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi imara na shirikishi na katika kuwawezesha wananchi kuishi maisha bora na ya kisasa. Bila kuwa na vyanzo ya uhakika vya upatikanaji wa umeme hapa nchini itakuwa ni ndoto kupata maendeleo ya kiteknolojia, ambayo kwa sasa ndio msingi wa ukuaji uchumi na kichocheo cha maisha bora.

5.4 Madini

5.4.1 Hali halisi ya madini nchini

Nchi yetu imejaliwa madini ya kila aina, ikiwemo almasi, dhahabu, uranium na Tanzanite, kutaja kwa uchache tu. Hata hivyo, madini haya hayajatusaidia sana kwa

sababu Serikali ya CCM imekabidhi na kukasimisha utafutaji na uvunaji wa madini haya mikononi mwa wageni. Matokeo yake, pamoja na kwamba mapato yatokanayo na madini yamechangia sana katika kuonyesha kuwa uchumi unakuwa, mapato haya hajasaidia nchi na wananchi kwa sababu sehemu kubwa yake yanakwenda nje na yanapotea kwa ufisadi. Vilevile, hakuna uhusishaji wa sekta ya madini pamoja na sekta zingine muhimu katika kukuza uchumi kama vile nishati na kilimo.

Mbaya zaidi ni kwamba madini haya yanayochimbwa sasa yatakwisha, na kwa kuwa serikali ya CCM haina mpango wowote wa kuweka akiba itokanayo na pato la madini haya, vizazi vijavyo havitakuja kuonja kamwe matunda ya mali asili za taifa. Madini lazima yatoke ardhini yaje juu ya nchi yaonekane kwa minajili ya miundo mbinu iliyotengeneza (barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, mipango miji, maji), kwa elimu iliyoongeza (mashule, vyuo na vyuo vikuu), afya iliyoboresha (mahospitali na watendekazi wake), kwa kilimo ilichoboresha na kwa viwanda vinavyozalisha. Hivi ndivyo nchi nyingi, ikiwemo Norway, Botswana na Afrika ya Kusini ilivyofanya.

Kwa ufupi, uchumi wa Tanzania ni uchumi uliolala (sleeping economy). Maana yake ni kuwa kile ambacho tunakiona kama ni shughuli mbalimbali za kiuchumi nchini ni kiduchu tu ya kile kinachowezekana kufanyika katika taifa letu. Lakini zaidi ni kuwa uchumi wetu ni uchumi wa bandia (artificial economy). Hii ina maana ya kwamba kutokana na vitendo vya kifisadi ambavyo vimekithiri katika shughuli mbalimbali za kiuchumi hadi ngazi za juu kabisa ya vyombo vya serikali, kile kinachoripotiwa katika vipimo mbalimbali hakiakisi ukweli hasa wa kiuchumi nchini. Hivyo, kutokana na hayo mawili uchumi wa Tanzania unahitaji kuamshwa na kusahihishwa ili uweze kuwa kweli uchumi wa kisasa na wenye kukua kutakakooneshwa na vipimo vya uhakika vya uchumi.

CHADEMA inaamini ina uongozi makini ambao pindi ukiingia madarakani mwezi Novemba itaanza kuandaa na hatimaye kutekeleza mipango madhubuti ya kuamsha uchumi pamoja na kuusahihisha ili uchumi wetu uwe wa kisasa zaidi na wenye kuonesha kwa usahihi shughuli mbalimbali za uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali.

5.5 CHADEMA itafanya nini kuboresha na kuimarisha uchumi?

5.5.1 Ili kuimarisha na kuboresha uchumi, Serikali ya CHADEMA itaweka mkazo katika mambo yafuatayo:

- Kubana matumizi ya serikali kwa kuachana na matumizi ya anasa na yasiyo na umuhimu kwa taifa kama msusuru wa magari ya maafisa, warsha, makongamano na safari zisizo za lazima na kuunda serikali ndogo inayozingatia tija ya matumizi ya fedha,ufanisi na utendaji. Katika kupunguza matumizi ya serikali, CHADEMA itafanya yafuatayo:

- Itapunguza mishahara na posho za viongozi wote wa juu wa kisiasa kuanzia Rais, hadi wakuu wa mikoa kwa asilimia 20. Mishahara na posho za wabunge zitapunguzwa kwa asilimia 15 huku mishara na posho ya watendaji wote na wakuu wa mashirika na taasisi za umma itapunguzwa kwa asilimia 15.

- Rais Slaa hatofanya safari ndefu za nje katika mwaka wa kwanza wa Urais wake. Ukiondoa safari za Baraza la Umoja wa Mataifa ambapo ni nafasi ya kukutana na kufahamiana na viongozi wengine duniani na za nchi majirani zetu, safari nyingine zote zitafanywa na viongozi wengine na kwa utaratibu utakaozingatia maslahi ya nchi, gharama, na faida inayopatikana kwa safari husika.

- Misafara yote ya viongozi wa juu wa serikali na taasisi zake zitawekewa utaratibu ili kuhakikisha kuwa ni watu wale tu wanaotakiwa kuwepo kwenye ziara hizo wanashiriki. Lengo ni kuhakikisha kuwa ziara za kiserikali hazitumiki kama mitaji ya posho.

- Kutokana na ukweli kuwa serikali imekuwa ikitenga kiwango kikubwa sana cha fedha katika posho ni muhimu serikali mpya kubadilisha utaratibu huo ili hatimaye kuinua mishahara ya watumishi wa umma. Kwa mfano, serikali ya CCM katika mwaka 2008/2009 ilitenga zaidi ya shilingi bilioni 509 (zaidi ya nusu Trilioni) kwa ajili ya posho mbalimbali. Hii ni sawa na malipo ya mwaka mzima ya walimu zaidi ya 109,000! Taarifa zinaonesha kuwa Ofisi ya Rais ndiyo inaongoza kwa posho hizo ikijigawia zaidi ya shilingi bilioni 148 kwa mwaka wa

2009/2010 na Bunge ikijigawia zaidi ya shilingi bilioni 36 katika kipindi hicho hicho.

- Serikali ya CHADEMA itaweka utaratibu ili semina, warsha na mafunzo katika taasisi mbalimbali za umma yanafanyika ndani na katika wakati wa kazi na bila uwepo wa posho maalum za “vikao za siku”. Mafunzo au mikutano yoyote itakayofanyika nje ya vituo vya kazi itahesabiwa ni sehemu ya kazi na serikali italipia na kurudisha gharama za safari, hoteli na posho ya kujikimu. Utaratibu mkali wa kisheria utawekwa ili kuzuia ulaghai wa aina yoyote na kuhakikisha wale wote (wafanyakazi na watoa huduma) watakaoshiriki kuiibia serikali kwa nyaraka au risiti za uongo wanachukuliwa hatua mara moja ikiwemo kuachishwa ajira. Lengo ni kupunguza posho hizi kwa zaidi ya asilimia 80 zikiendana na nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma kuendana na ujuzi, nafasi, na vyeo vyao kazini. Tunataka wafanyakazi wetu walipwe kwa haki kwa kile wanachofanya kwa haki.

- Kupanua wigo wa mapato yatokanayo na kodi, ikiwemo kufuta misamaha holela ya kodi isiyolenga katika kuboresha na kukuza uchumi. Kodi zote za bidhaa na huduma zitakazotozwa nchini zitakuwa na lengo moja kubwa nalo ni kuipatia serikali mapato.

- Kuchochea ukuaji wa kilimo cha kisasa, kibiashara na bora. Kimsingi kilimo kitaboreshwa na kutumika kama daraja la kuingia kwenye uchumi wa viwanda na huduma wenye fursa nyingi na tija (tazama maelezo zaidi katika sura inayohusu kilimo).

- Kuwaruhusu wakulima kuuza mazao ndani na nje ya nchi ili kujiongezea kipato na kuchangia zaidi katika pato la taifa.

- Serikali kuingia moja kwa moja katika utafutaji na uvunaji wa madini pamoja na raslimali zingine asilia kwa kushirikiana na makampuni ya kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha kuwa nchi inafaidika na raslimali za taifa. Katika kila mkataba

serikali utakaingia na sekta binafsi, iwe ya nje au ndani, itahakikisha inahodhi si chini ya asilimia 50 ya umiliki wa hisa.

- Serikali ya CHADEMA itaanzisha mfuko wa madini utakaotokana na mapato yatokanayo na madini. Mfuko huu utatunzwa katika benki kuu kwa muda wote wakati wa upatikanaji wa madini na utakuwa ni akiba na kumbukumbu ya raslimali kwa ajili ya matumizi ya vizazi vijavyo. Thamani ya madini yote kabla ya kuuzwa nje ya nchi yatapita benki kuu na kuthaminiwa thamani yake, kama akiba ya fedha za taifa.

- Uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo vinavyotoa ajira kwa wingi. Ili kufanikisha hili:

    - Serikali ya CHADEMA itaanzisha mfumo wa utoaji wa elimu ya kufundisha wajasiriamali kupitia vyuo vya ufundi.

- Benki teule zitapewa motisha na masharti ya kukopesha wazalishaji na wenye viwando vidogovidogo.

- Ili kupunguza msongano katika Bandari ya Dar es Salaam, sambamba na kuifanya Dar es Salaam ipumue, tutaimarisha bandari za Mtwara na Tanga kwa kuzifanya zifanye kazi kibiashara na kwa kuzingatia maslahi ya kitaifa. Aidha, tutaanza mkakati wa kuziunganisha bandari hizi tatu na nchi za jirani zitakazozihudumia; Bandari ya Mtwara kwa nchi za Kusini, Bandari ya Dar es Salaam kwa nchi za kati, na Bandari ya Tanga kwa nchi za Kaskazini.

5.5.2 Mpango wetu maalumu wa 'kumijishisha' vijiji

Ukuaji wa uhakika wa uchumi unategemea, pamoja na mambo mengine, ukuaji wa miji na uwepo na huduma muhimu za kiuchumi na kijamii zinachochea ukuaji wa miji katika sehemu mbalimbali za nchi. Kwa muda mrefu, tangu nchi yetu ipate uhuru, pamekuwepo na uwiano usiolingana wa ukuaji miji kiasi kwamba maeneo mengi ya nchi yameendelea kudorara na machache tu ndio yakikua. Katika miaka kumi iliyopita tumeshuhudia

ongezeko la idadi ya watu jijini Dar es Salaam usioendana na ukuaji wa miundo mbinu na huduma zingine muhimu za kijamii.

Hii imesababishwa, pamoja na mipango mibovu ya miji, na uwepo wa huduma nyingi jijini Dar es Salaam ambazo hazipatikani kwingineko hapa nchini. Kuna haja basi ya kuifanya Dar es Salaam ipumue kwa kuchochea miji mingine kukua ili watu wavutike kuishi huko. Hili linahitaji uwekezaji wa makusudi na wa kimkakati kwenye huduma muhimu kama vile miundo mbinu, nishati na maji. Hivyo basi, sambamba na kuimarisha huduma muhimu za kijamii jijini Dar es Salaam, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo katika ‘kumijishisha’ au ‘kudaramisha’ miji na maeneo ya vijini hapa nchini:

- Kuwekeza katika nishati ya umeme ili kupanua wigo wa watumiaji wa umeme nchini kutoka asilimia 15 (15%) ya sasa hadi angalau asilimia hamsini (50%) na vijiji kutoka asilimia moja (1%) ya sasa hivi hadi asilimia 25 (25%) ifikapo mwaka 2020

- Kuchochea ujenzi wa viwanda vidogo vidogo vya usindikaji vya kikanda. Serikali ya CHADEMA inakusudia kuanzisha kiwanda kimoja cha usindikaji katika kanda tatu kufikia mwaka 2015.

- Kuwekeza katika uchimbaji wa gesi asilimia na kuanzisha mfumo wa gridi ya gesi ili kupanua vyanzo vya nishati.

- Tutawekeza katika miundo mbinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, umeme na maji kikanda kuanzia Mtwara hadi Mwanza, ikiwemo:

    - Kuboresha usafiri wa reli ya kati na reli ya Tanga, Moshi hadi Arusha ili hatimaye iweze kuwa njia ya haraka, nafuu na ya starehe katika ya miji hiyo na Dar. Hii itakuwa ni pamoja na kurudisha Mamlaka ya Reli ya Tanzania (TRA) na kuhakikisha mamlaka hiyo inajiendesha kibiashara kwa kushirikiana na sekta binafsi.

    - Kupanua barabara ya Dar-Chalinze kwa kuiweka katika njia sita (six lanes road) ndani ya miaka mitano ya utawala wa Serikali ya CHADEMA. Eneo

la Kibaha ambapo pamekuwa pakitokea ajali nyingi pataangaliwa mara moja baada ya CHADEMA kuingia madarakani ili hatimaye suluhisho la kisayansi na la haraka lipatikane na kuepusha ajali katika eneo hilo.

- Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mbeya-Mwanza, na kujenga reli itakayounganisha Mtwara na Iringa.

SURA YA SITA

6. KUJENGA UONGOZI BORA NA MFUMO MPYA WA UTAWALA

6.1 Utangulizi

Uongozi bora na utawala wa sheria, pamoja na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma, ni nguzo ya msingi katika kukuza uchumi wa taifa lolote duniani. Nchi zote zilizoendelea zina sifa ya kukumbatia utawala bora na utawala wa sheria, na nchi nyingi maskini ni nchi ambazo pia hazina demokrasia, zina utawala wa imla, zinatesa watu wao, hazina utawala bora na haziheshimu utawala wa sheria. Kwa hivyo, ni muhimu kutambua kwamba ili tuweze kupiga hatua ya kweli ya maendeleo, hatuna budi kujenga na kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria.

Ili kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria, ni muhimu kuweka na kudumisha uwiano thabiti katika mgawanyo wa madaraka miongoni mwa mihimili ya utawala, yaani dola, bunge, mahakama na taasisi za kiraia. Aidha, ili kuimarisha utawala bora na uwajibikaji, ni muhimu kuwepo mamlaka kamili ya kiutawala na kiutendaji katika ngazi za chini.

Tafiti zinaonyesha kuwa kushindwa kuutokomeza umaskini hapa nchini kunasababishwa na, pamoja na mambo mengine, mipango isiyoshirikishi pamoja na kutokuwepo utawala ubora na utawala wa sheria na kutokuwepo uwajibikaji miongoni mwa viongozi wa kisiasa na watumishi wa umma, sambamba na ukweli kwamba serikali ya awamu ya nne iliingia madarakani kwa kutumia fedha za kifisadi, na hivyo kulazimika kujiendesha kifisadi.

6.2 CHADEMA imegawa matatizo ya utawala bora na utawala wa sheria katika makundi matatu yafuatayo:

6.2.1 Kutokuwepo mgawanyo kamili wa madaraka miongoni mwa mihimili ya utawala. Badala yake serikali kuu imehodhi madaraka ya utawala. Bunge letu limeendelea

kuwa chombo cha kubariki maamuzi ya serikali badala ya kuwa chombo cha kuisimamia na kuiwajibisha serikali. Maamuzi ya mahakama hayaheshimiwi ipasavyo, na taasisi za kiraia zinaendelea kuwa dhaifu kwa kuwa zimebanwa kisheria na zimeingiliwa na mamluki na mawakala wa serikali. Vyama vya wafanyakazi vimeendelea kuwa dhaifu kwa kuwa vinatishwa na kujengewa mazingira magumu ya kiutendaji.

6.2.2 Serikali kuu imeendelea kuwa kubwa na kusababisha gharama za utawala kuwa kubwa. Kutokana na ukubwa wa serikali, fedha zinazokusanywa kutoka kodi za wananchi zinaishia kugharamia utawala. Bado mfumo wetu wa utawala unatumia nguvu kazi nyingi sana kuzalisha kitu kidogo.

6.2.3 Mfumo wa utawala umeweka mazingira ambapo vyombo mbalimbali vya kiutendaji wa kiserikali vimekuwa vikiingiliwa na wanasiasa (politicization of public service) kunakosababisha vyombo hivi kushindwa kutenda haki kwa mujibu wa kanuni za utendaji na utawala wa sheria. Matokeo yake viongozi wa kisiasa wamekuwa na ushawishi usiotakikana katika utendaji wa vyombo vya umma. Hili ni lazima likomeshwe.

6.3 Matokeo ya matatizo haya katika utumishi wa umma ni pamoja na haya yafuatayo:

6.3.1 Watumishi wa umma kuwa na morali mdogo wa kazi na kukosa uzalendo, kunakosababisha utendaji dhaifu na vitendo vya ubadhirifu wa mali ya umma na ufisadi. Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na Benki ya Dunia unaonyesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zilikubwa na tatizo la kile kinachoitwa ‘Rushwa ya Kimya’ (Silent Corruption). Hii ni rushwa ambayo watendaji wa umma hawakai maofisini na muda mwingi wa kazi wanautumia kwa kazi za binafsi badala ya kutoa huduma kwa wananchi

6.3.2 Kukithiri kwa vitendo vya ufisadi ambavyo vimehusisha na vinaendelea kuhusisha taasisi za umma kwa upande mmoja na viongozi wa kisiasa, jamaa na

marafiki zao kwa upande mwingine huku mwathirika wa ufisadi akiwa ni Mtanzania wa kawaida.

6.3.3 Kukosekana uzalendo, uadilifu, umakini na upeo miongoni mwa viongozi wa kisiasa kunakosababishwa na kukosekana mfumo imara wa kupika viongozi wa kitaifa.

6.3.4 Gharama ya maisha kupanda kwa kiasi kikubwa kwa sababu wale wanaopata fedha za kifisadi (rushwa, hongo au nyinginezo) hawajali gharama ya huduma na bidhaa mbalimbali. Matokeo yake soko linauza bidhaa na huduma mbalimbali kwa bei ya juu sana kuliko uhalisia kwa sababu wanunuzi wenye fedha za ufisadi wapo. Matokeo ya hili ni kuwa hata wale wenye pesa halali zinazotokana na jasho lao wanajikuta wanatumia fedha nyingi kupata huduma na bidhaa mbalimbali lakini mwananchi wa kawaida akiendelea kujikuta akibangaiza maisha yake na kuishi kwa mtindo wa siku kwa siku.

6.4 CHADEMA itafanya nini katika kujenga uongozi bora na kuimarisha utawala wa sheria?

6.4.1 Ili kuimarisha kujenga uongozi na kuimarisha utawala bora na utawala sheria, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

i) CHADEMA inatambua kwamba nguvu ya utawala bora ni KATIBA ya nchi iliyojengwa katika misingi ya kulinda demokrasia, kulinda haki za wananchi na kutoa fursa kwa wananchi hao kuwawajibisha viongozi wao. Katiba yetu ya sasa haikujengwa katika misingi hii. Kwa sababu hii, hatua ya kwanza itakayochukuliwa na CHADEMA ndani ya siku 90 tangu kuchaguliwa kwake ni kuanzisha mara moja mchakato wa kubadilisha katiba ili hatimaye tupate katiba ambayo imejengwa katika misingi ya kidemokrasia na haki za binadamu. Lengo ni kuhakikisha kuwa inapofika uchaguzi mkuu mpya wa 2015, Tanzania inafanya uchaguzi huo chini ya Katiba mpya ambayo, pamoja na mambo mengine,

itakaweka mgawanyo thabiti wa madaraka baina ya Bunge, Serikali na Mahakama.

ii) Ili kupunguza gharama za utawala na kutoa madaraka na mamlaka katika ngazi za chini, Serikali ya CHADEMA itapunguza ukubwa wa serikali kuu na kuimarisha madaraka katika ngazi za halmashauri ya Wilaya. Wizara za Serikali zitatamkwa kwenye Katiba ya nchi ili kuondoa mwanya wa Rais kubadilisha wizara kila anapojisikia kufanya hivyo. Tutafuta vyeo vya wakuu wa wilaya na kuimarisha mamlaka katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji. Tutaanzisha mchakato wa kupeleka madaraka makubwa ya kiutendaji na kiutawala mikoani ili kuchochea maendeleo.

iii) Ili kukabiliana na wimbi la ufisadi miongoni mwa viongozi wa kisiasa na watumishi wa umma, Serikali ya CHADEMA itafanyia mabadiliko ya haraka sheria ya Maadili ya Umma ili hatimaye watumishi wote wa Umma wakumbushwe kuwa wako katika utumishi wa umma. Katika sheria hii adhabu kali zitawekwa ili kuhakikisha kuwa watumishi wa umma hawatumii vyeo na nafasi zao vibaya ili kujinufaisha wao au watu wa karibu yao. Sheria hii itakuwa tayari kwenye Bunge la Kwanza litakalokuwa chini ya CHADEMA.

iv) Ili kuimarisha utendaji wa Tasasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Serikali ya CHADEMA itaiondoa taasisi kutoka ofisi ya Rais na kuifanya huru chini ya Katiba. Pamoja na kwamba Rais atamteua Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, uteuzi wake hautakamiliki hadi utakapojadiliwa na kuthibitishwa na Bunge. Aidha ukomo wa utumishi wa Mkurugenzi wa TAKUKURU utakuwa kwa mujibu wa Katiba, na sio matakwa na utashi wa Rais. Kwa maneno mengine Mkurugenzi wa TAKUKURU hatoweza kuondolewa na Rais isipokuwa kwa utaratibu uliowekwa wazi kisheria.

v) Viongozi wate wa kisiasa na watumishi wa umma ambao walishabainishwa kujihusisha na ufisadi na ubadhirifu (***rejea orodha ya mafisadi***) ya umma lakini Serikali ya CCM imeshindwa kuwafikisha mahakamani kwa kuwa ni washiriki, watafikishwa mahakamani ndani ya siku 180 chini ya Sheria ya Kuzuia Mitandao ya Uhalifu na Uhujumu Uchumi ya 1984 pamoja na Sheria nyingine zozote ambazo zitaonekana zimevunjwa. Wale watakaothibitika mahakamani kuhusika na vitendo vya ufisadi, pamoja na kuadhibiwa na mahakama, mali zao zitataifishwa na kurudishwa serikalini. Katika hili viongozi waliopita (wakiwemo Marais) ambao wataonekana kuhusika na vitendo vyovyote vya ufisadi au uvunjaji wa sheria watavuliwa kinga zao na Bunge ili hatimaye waweze kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka dhidi yao yatakayoletwa na Taifa lao. Hakutakuwa na kiongozi ambaye hatoweza kufikishwa mahakamani kama amefanya vitendo vya uhalifu akiwa madarakani.

vi) Kutokana na kukithiri kwa vitendo vya kifisadi miongoni mwa viongozi wa kisiasa na watumishi wa umma hapa nchini, na kwa kuzingatia uwezo mdogo wa mahakama zetu katika kushughukikia kesi zinazohusu ufisadi, Serikali ya CHADEMA itafanya uteuzi wa kutosha wa Majaji wa Mahakama Kuu ili baadhi yao wakae kama Mahakama ya Hujuma ya Uchumi kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia Mitandao ya Uhalifu na Uhujumu Uchumi ya 1984. Lengo ni kuhakikisha kuwa kesi zote kubwa za ufisadi zinashughulikiwa kwa haraka bila kuingilia utendaji wa mahakama katika kesi zinazohusu makosa mengine.

vii) Ili kujenga moyo wa kuheshimu maadili katika ajira na kazi mbalimbali vyuo vikuu nchini vitatakiwa katika masomo yake ya msingi kuwepo na masomo ya mambo ya maadili na miiko (morality and ethics). Katika ngazi za chini za elimu masomo yenye kuchochea uzalendo yatatolewa kama sehemu ya elimu ya Uraia.

viii) Kwa kuwa vijana ndio kundi kubwa hapa nchini, na kwa kuwa uhai wa muda mrefu wa taifa letu upo mikononi mwa vijana, Serikali ya CHADEMA

itawezesha vijana kuunda Baraza la Vijana (BAVITA) ambalo limekwamishwa na Serikali ya CCM kwa muda mrefu. Baraza hili litakuwa na jukumu la kuwaunganisha vijana wote nchini bila kujali itikadi zao za kisiasa au dini zao. Baraza hili pia litawezeshwa ili ndio liwe tanuru la kupika viongozi wa nchi. Jukumu la Baraza hilo litakuwa pia kama chombo cha mijadala na mafunzo mbalimbali ya vijana nchini na kusimamia ujirani mwema, umoja na ushirikiano katika utendaji wa mambo mbalimbali.

ix) Ili kuwawezesha wanawake kuunganisha nguvu zao bila kujali itikadi zao za kisiasa, Serikali ya CHADEMA itaruhusu na kufanikisha kuanzishwa kwa Baraza la Wanawake Tanzania. Baraza hili litakuwa chombo huru cha kutetea maslahi ya wanawake wote na wasichana nchini.

SURA YA SABA

7. FURSA KWA KILA MTANZANIA KUPATA AJIRA, UJIRA BORA, MFUMO WA PENSHENI NA HUDUMA KWA WAZEE

7.1 Utangulizi

Ajira ni shughuli inayomwezesha mtu kuzalisha pato kwa ajili ya kujikimu kimaisha. Kuna nguzo kuu mbili katika kupata ajira. Nguzo ya kwanza ni elimu aliyo nayo mtu, kwani hii ndiyo humpa maarifa na ujuzi wa kufanya kazi za kuzalisha kipato. Nguzo ya pili ni uchumi wa nchi ambao ndiyo huzalisha kazi na kuwapatia watu mapato kuweza kununua bidhaa au huduma zinazozalishwa/zinazotolewa.

Kwa hiyo tunapozungumzia upatikanaji wa ajira kwa kila mtanzania, sisi CHADEMA tunazungumzia mambo makubwa mawili ambayo ni :

- Kuboresha mfumo wa elimu utakaotoa wahitimu wenye soko la kitaaluma na ujuzi katika nyanja zote za uchumi wa taifa
- Kuimarisha misingi mama ya uchumi itakayotoa fursa nyingi za kazi kwa Watanzania wenye fani katika nyanja zote za Uchumi

Kuna aina mbili kuu za ajira. Aina ya kwanza ni ajira ya kujitegemea kwa kufanya shughuli au kuanzisha shughuli binafsi za kiuchumi. Ajira ya aina hii inaweza kuwa ya kujipatia mahitaji binafsi ya kujikimu kimaisha au ya kuzalisha zaidi kwa kuuza na kuleta fedha kwa mahitaji mengine ya maisha. Watu wa aina hii huitwa watu (waliojiajiri) na kwa kujiajiri kwao wanaweza pia kuzalisha fursa za vijana kwa watu wengine. Ajira ya aina ya pili ni ile ya kuajiriwa kwa mkataba wa kulipwa ujuzi na mwajiri wa kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi. Ajira za aina hii hutolewa na sekta ya umma na sekta binafsi.

Miaka mitano iliyopita, Serikali ya CCM iliahidi kumaliza tatizo la ajira miongoni mwa vijana. Malengo ya MKUKUTA I ilikuwa ni kupunguza tatizo la ajira kutoka asilimia 12.9 mwaka 2000/2001 hadi kufika asilimia 6.9 ifikapo mwaka 2010. Hata hivyo, hali

halisi ni kwamba tatizo la ajira limepungua kwa asilimia mbili tu kutoka asilimia 12.9 hadi asilimia 11 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2010.

Tatizo kubwa zaidi katika ajira ni kwamba asilimia 88 ya Watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi hawamo katika mfumo rasmi wa ajira. Hawa ni watu waliojiajiri wenyewe katika ajira zinazoitwa za mashaka kama vile kuuza maji barabarani, kupaka rangi viatu, umachinga, n.k. Kwa hakika hili ni bomu linasubiri kulipuka na tatizo ambalo Serikali ya CCM haina majibu, na kwa kweli inafurahia hali ya sasa kwa sababu ndio msingi wake wa kubaki madarakani. Na kwa sababu wafanyakazi walio katika mfumo rasmi ni wachache wasiozidi laki tano, ndio maana Rais Kikwete amekuwa na kiburi cha kuwadharau wafanyakazi hao hata kuwaambia kwamba hahitaji kura zao na wala hatabadilisha kima chao cha chini hata wakidai kwa miaka nane ijayo!

7.2 CHADEMA itafanya nini kukuza ajira na ujira bora?

7.2.1 Kuhusu ajira na ujira bora

CHADEMA inatambua umuhimu wa ajira ya uhakika katika kuhakikisha ustawi wa wananchi, jamii na taifa kwa ujumla. Matatizo ya ajira yapo katika makundi makuu mawili. Mosi, ni ufinyu wa ajira katika mfumo rasmi kunakosababisha watu wengi kuwa na ajira za mashaka. Pili, uduni wa malipo ya wafanyakazi waliopo katika mfumo ulio rasmi, na hasa wa sekta ya umma kunakosababisha utendaji dhaifu na kukithiri kwa vitendo vya ufisadi na wizi wa mali ya umma.

Kuhusu ajira hafifu katika mfumo rasmi, kuna sababu tatu za msingi zinasababisha uhaba wa ajira ya uhakika na ujira bora hapa nchini, ambazo ni ukuaji mdogo wa uchumi, uzalishaji duni viwandani na ukosefu wa maarifa na stadi stahiki miongoni mwa vijana. Ili kuongeza ajira na kuboresha ujira, serikali ya CHADEMA itaweka mkazo katika:

- Kuinua uchumi kwa kutekeleza mipango mbalimbali ya ujenzi wa miundo mbinu.
- kupanua na kuimarisha viwanda vidogovidogo na

- kuimarisha elimu ya ufundi na stadi za maisha kwa vijana.

Kuhusu uduni wa malipo na mafao madogo katika mfumo ulio rasmi, na hasa katika sekta ya umma, serikali ya CHADEMA itaweka mkazo katika mambo yafuatayo:

- Tutaongeza pato la mshahara ili kuhakikisha kuwa mfanyakazi anapata kiwango ambacho kinakidhi mahitaji ya maisha katika mazingira yetu. Ili kuondoa manung'uniko ya mara kwa mara kwa wafanyakazi yanayohusu mishahara na marupurupu, Serikali ya CHADEMA itaanzisha utaratibu wa kupandisha mishahara kwa kutumia kanuni inayoendana na ongezeko la mfumuko wa bei na upandaji wa gharama za maisha. Hii inamaanisha kuwa mishahara itapanda kulingana na kupanda kwa mfumuko wa bei na gharama za maisha.

- Tutakomesha pengo lililojengwa la utofauti wa mishara miongoni mwa watumishi wa umma. Pengo la kipato linasababisha manung'uniko na kukata tama miongoni mwa watendaji wa sekta umma, kunakosababisha udokozi, rushwa na hatimaye wizi wa mali za umma.

- Ili kumpunguzia mzigo wa kodi wafanyakazi, ambao wanalipa kodi nyingi zaidi kuliko wananchi wengine, tutapunguza kodi ya pato itokanayo na mshahara(PAYE) kutoka asilimia 14 ya sasa hadi asilimia 10.

- Tutatoa msukumo na kipaumbele kwa wafanyakazi wanaotoa huduma muhimu za jamii kama vile walimu, madaktari na wauguzi. Mishahara na posho za walimu na watumishi wengine katika huduma nyeti za afya wa maeneo ya mikoa iliyonyuma kimaendeleo haitakatwa kodi ya mapato (PAYE). Mikoa hiyo ni Mtwara, Lindi, Kigoma, Manyara, Rukwa na Katavi.

7.2.2 Kuhusu mfumo wa pensheni na huduma kwa wazee

Mfumo wetu wa ulipaji wa pension nchini una mapungufu mengi sana . Baadhi ya mapungufu haya ni ; idadi ndogo ya Watanzania ambao wameandikishwa katika mifuko ya hifadhi jamii , mafao duni kwa walengwa, tofauti kubwa ya mafao kwa makudi

mbalimbaliya wastaafu na hivyo kujenga matabaka, kutoratibiwa kwa mfumo mzima na hivyo kuruhusu kila mfuko kufanya kila unachoamua na kutowashirikisha kikamilifu na kuwanyima mamlaka ya kutoa maamuzi wachangiaji katika mifuko hiyo.

Ili kuboresha mfumo wa pensheni kwa wazee, Serikali ya CHADEMA inakusudia kufanya yafuatayo:

a) Kuboresha mfumo wa utoaji pension (contributory pension) kwa :

1. Kuanzisha utaratibu utakaowawezesha wachangiaji katika mifuko hii kuwa na sauti katika uendeshaji wa mifuko husika kwa kuteua wawakilishi katika bodi zinazosimamia mifuko hiyo
2. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa mifuko hii na utoaji wa pensheni nchini na kuwa na mafao bora na yanayowiana.
3. Kupanua wigo wa mifuko hii kwa kusajiri wafanyakazi /watu wengi katika sekta binafsi.

b) Kuanzisha pension jamii kwa wazee wote (universal social pension)

Kuna wazee takribani 2.1 milion katika nchi yetu. Asilimia 82 ya wazee wote nchini wanaishi vijijini. Mpaka sasa ni asilimia 4 ya wazee wote nchini wanaopata pensheni. Wazee hawa ni wale ambao walikuwa wameajiriwa katika ajira rasmi. Mbili ya tatu ya wapatao pensheni kwa sasa ni wanaume. Asilimia 96 ya wazee wote kwa sasa (wengi wao wakiwa ni wakulima na wafugaji hawana pensheni ingawa nao wamechangia kwa kiasi kukubwa kulijenga taifa letu. Takribani asilimia 30% ya walemavu wote ni wazee. Takwimu zinaonyesha kuwa kaya zilizo na wazee (ambazo ni karibia robo ya kaya zote nchini) ni maskini sana. Kiwango chao cha umaskini katika kaya hizi kiko juu kwa asilimia 22.4, ukilinganisha na wastani wa umaskini wa taifa (40.9 %) ukilinganishwa na asilimia 33.4 ambayo ni wastani wa taifa.

Wezee hawa wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo kuwatunza asilimia 50 ya watoto yatima nchini katika kipindi ambacho wao wenyewe wanahitaji kutunzwa, kushindwa kupata mahitaji muhimu kama chakula cha kwao na wategemezi wao,

kushindwa kupata huduma za afya bure kama ilivyokubaliwa na serikali, kuuawa kwa tuhuma za uchawi. Inakadiriwa kuwa zaidi ya wazee 300 wanauawa kila mwaka kwa tuhuma za uchawi.

Umaskini uliokithiri kwa wazee wengi unawafanya kushindwa kuzifikia huduma muhimu ambazo zinatolewa na serikali kwa ajiri ya makundi maskini. Mfano wazee kukosa nauli ya kusafiri kufika hospitali hata kama huduma hospitali zinatakiwa kutolewa bure, watoto wanaolelewa na wazee kutoweza kusoma vizuri kwa kukosa mahitaji muhimu kama vile chakula, sare , vitabu , nauli kwenda shuleni nk- hata kama serikali imeondoa karo katika shule za masingi, kushindwa kujipatia hata pembejeo ambayo tayari imewekewa ruzuku na serikali kwa vile hawawezi kulipia kiwango wanachotakiwa kuchangia, na kushindwa kujiunga na SACCOS kwa vile hawawezi kulipia mchango wa awali . Moja ya motokeo yaliyo dhahili ni wazee kuwa ombaomba mitaani wengi wao wakiongozwa na wajukuu wao. Wazee kukosa wawakilishi waliowachagua wao katika vyombo vya maamuzi kama serikali za vijiji, kata, halmashauri na bunge kama walivyo wanawake, na sera ya taifa ya wazee (2003) kutotungiwa sheria imechangia kwa kiasi kikubwa kudidimia kwa maisha ya wazee.

Kwa kutambua ukweli huu na kwa kuzingatia kwamba katiba ya nchi ibara ya 11(i) inatambua haki ya kila mtu kupata hifadhi ya jamii wakati wa uzee CHADEMA unakusudia kufanya yafuatayo:

i) kuazisha mfumo wa utoaji pension kwa wazee wote (non contributory- universal social pension)

Malipo ya pensheni (universal social pension) yatatolewa na serikali kwa kila raia wa nchi hii ambaye atakuwa amefikia umri wa kuitwa mzee (miaka 60) kwa mujibu wa sera ya taifa ya wazee . Ili kugharimia mfuko huu taifa litatenga kiasi kisichopungua asilimia 1 ya GDP kila mwaka kwa ajiri ya mfuko huu.

Matokeo ya utafiti wa hivi karibuni unaonyesha *(A study into the feasibility of a universal social pension May 2010*) kuwa utoaji wa pension kwa wazee wote utachangia kwa kiwango kikubwa kupunguza umaskini kwa wazee na wategemezi wao wakiwamo

nusu ya yatima wote hapa nchini. Hivyo basi, Serikali ya CHADEMA itatenga fedha katika bajeti ya 2011/2012 ili kutoa kiwango cha Tsh 15,000/= kwa mwezi kwa kila mzee (mtu yeyote mwenye umri wa miaka 60 na kuendelea). Kiwango hiki kitafanyiwa mapitio kipindi kwa kipindi. Hatua hii itapunguza umaskini miongoni mwa wazee kwa asilimia 57.9. Zaidi ya yote, mfumo wa pensheni kwa wazee wote itanufaisha takribani asilimia 25 ya kaya zote nchini (robo ya Watanzania) na hivyo kupunguza wastani wa kiwango cha umaskini cha taifa kwa asilimia 11.9% ((kutoka 33.4% - 29.4% cha sasa).

ii) ***Serikali ya CHADEMA pia itatunga sheria itakayowawezesha utoaji wa matibabu bure kwa wazee wote*** . Katika kutekelezeka bila usumbufu wowote, na kuwaruhusu wazee kuwa na mwakilishi angalau mmoja waliomchagua wao katika vyombo vya maamuzi (serikali za kijiji, kata, halmashauri na bunge) ili mawazo yao yapate kuwakilishwa kwa ukamilifu wakati wote.

iii) ***Serikali itapitia upya sera ya taifa ya wazee*** na kuiboresha na kuitungia kanuni zitakazosaidia utekelezaji wake .

iv) ***Juhudi mahususi zitafanyika kudhibiti mauaji ya wazee*** na kuagiza vyombo husika kufanya uchunguzi wa kesi za mauaji zilizopo kwa haraka na kukamiliha kesi zilizoko mahakamani.

SURA YA NANE

8. KUIMARISHA ULINZI NA USALAMA

8.1 Utangulizi na hali halisi

Kazi ya msingi kabisa ya serikali yeyote dunia inayojali watu wake ni kulinda maisha na mali za raia, pamoja na kuhakikisha kuwa mipaka ya nchi ipo salama. Pamoja na kwamba majeshi yetu ya ulinzi na usalama yanafanya kazi nzuri bado kuna changamoto nyingi zinazoyakabili majeshi haya na kushindwa kufanya kazi yao kikamilifu na kwa ufanisi. Kutokana na hili, usalama wa nchi, raia na mali bado upo katika mashaka makubwa.

Vyombo vyote vya ulinzi vinakabiliwa na changamoto kubwa sana ambazo pasipo kuangaliwa kwa haraka kutasababisha kulega lega kwa mfumo wetu wa usalama na kusababisha matatizo katika utendaji wa nchi na maisha ya watu wake.

Katika miaka ya karibuni, utendaji wa Usalama wa Taifa umedorora sana kutokana na kuingiliwa na wanasiasa wa chama tawala. Matokeo yake chombo hiki muhimu kimeanza kupoteza imani, heshima na hadhi yake katika jamii na kuanza kuonekana kuwa kipo hapo kwa ajili ya Usalama wa CCM na wanasiasa wake, badala ya usalama wa Taifa.

Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na jeshi la polisi kukabiliana na uhalifu nchini, mauaji ya raia wasio na hatia yanaendelea kutokea na wauaji hawakamatwi na kushughulikiwa kisheria ipasavyo, kutokana na changamoto nyingi zinalikabili jeshi la polisi, ikiwemo maslahi duni, mazingira magumu ya kazi na makazi na nyenzo duni za utendaji kazi. Kwa mfano, polisi wanaenda kupambana na majambazi bila vifaa kama vile vazi maalumu la kuzuia risasi (bullet proof). Aidha, wakati mawaziri na viongozi wengine wa chama tawala wanabadili magari ya kifahari kila mara, magari ya polisi ni machache na mengi yao yamechakaa.

Kwa kifupi vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimedhoofishwa na kufifishwa kiutendaji kwa kunyimwa fedha na vitendea kazi vya kutosha na kwa kuingiliwa kiutendaji na viongozi kisiasa wa chama tawala. Vyombo hivi vimejikuta vikifanya kazi zaidi kwa ajili ya kulinda maslahi ya chama tawala na viongozi wake badala ya kufanya kazi yao ya msingi ya kulinda taifa, raia wake na mali zao.

8.2 CHADEMA itafanya nini katika kuimarisha ulinzi na usalama?

Kwa kutambua changamoto mbalimbali zinazokabili vyombo vyetu vya usalama Serikali ya CHADEMA inakusudia kufanya mabadiliko makubwa ya mfumo wetu wa ulinzi na usalama ili hatimaye tuweze kujenga vyombo na mfumo wa kisasa wa kiusalama na kuondokana na mfumo wa zamani ambao bado una mabaki ya fikra za enzi za ukoloni na masalia ya vita baridi. Tanzania tunayoitaka ni lazima iwe tayari kulinda watu wake, uchumi wake na maslahi yake pasipo kuwa na hofu.

Hivyo basi, Serikali ya CHADEMA mara tu itakapoingia madarakani itachukua hatua zifuatazo ili kuanza mara moja mchakato wa kubadilisha na kuboresha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

8.2.1 Jeshi la Polisi

Serikali ya CHADEMA itaanza utaratibu wa kuliunda na kulipanga upya Jeshi la Polisi upya ili kulileta katika karne ya ishirini na moja likiwa jepesi zaidi, imara zaidi, la haraka zaidi na lenye nidhamu zaidi ya kijeshi. Kupanga huko kuna lengo la kulifanya jeshi letu ndani ya miaka mitano ya kwanza ya utawala wa CHADEMA kuwa jeshi bora zaidi la Polisi katika Bara la Afrika na linaloheshimika pote duniani.

Hivyo basi Serikali ya CHADEMA itaandaa mabadiliko ya kisheria ili kuligawa jeshi la Polisi katika sehemu kubwa mbili. Sheria ambazo zitafutwa au kufanyiwa mabadiliko ni pamoja na ile ya Police Force & Auxiliary Service Act, Kanuni za Adhabu, na sheria ya mambo ya silaha pamoja na Katiba yenyewe. Yote ni katika kuhakikisha kuwa tunajenga jeshi la Polisi la kisasa na lenye hadhi ya kimataifa.

Katika kuliimarisha Jeshi la Polisi kiutendaji, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

- Jeshi la Polisi la Taifa litakuwa na jukumu kubwa la kusimamia sheria za nchi na kupambana na uhalifu mkubwa kama itakavyoanishwa katika Sheria.

- Jeshi la Polisi la Taifa litakuwa na Madaraka ya Juu ya kipolisi sehemu yoyote nchini na wakati wowote. Hii ina maana Jeshi la Polici litaweza kuingilia na kufanya kazi ya kipolisi mahali popote inapohitajika au mahali ambapo jeshi la polisi la mkoa limeshindwa au linahitaji kuongezewa nguvu. Maafisa wa Jeshi la Polisi la Taifa watakuwa na madaraka ya juu ya kazi za kipolisi nchini.

- Jeshi la Polisi litakuwa linawajibika moja kwa moja chini ya Kamandi ya Polisi ya Taifa itakayoundwa na Inspekta Jenerali wa Polisi na Manaibu wake Wawili pamoja na Makamishna waandamizi wa taifa.

- Mkuu wa Jeshi la Polisi na Manaibu wake watateuliwa na Rais lakini hawatoshika nafasi zao hadi watakaposailiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge ambayo kwa kupiga kura itapeleka majina yao kwenye kikao cha Bunge zima ambalo litawapitisha.

- Makamanda wa Polisi wataweza kuondolewa tu kwenye nyadhifa zao kwa mujibu wa Sheria Mpya ya Jeshi la Polisi ambayo itazingatia kuwa viongozi wa kisiasa hawaingilii utendaji wa jeshi la polisi isipokuwa kwa mujibu wa sheria itakayowekwa wazi juu ya mahusiano hayo.

- Katika bajeti ya Polisi ya 2011/2012 serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa inatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Maabara ya kwanza ya kitaifa ya masuala ya Uhalifu (National Crime Laboratory) ya kisasa ya jeshi la Polisi nchini. Hii italeta vita dhidi ya uhalifu mbalimbali kuwa ni ya kisasa zaidi na yenye kuhakikisha wahalifu wanapatikana kwa njia za kisayansi na siyo kukisia au kutumia njia ambazo zimepitwa na wakati na ngumu kuweza kutumika kama

vidhibiti mahakamani. Ifikapo 2015 kutakuwa na maabara nyingine tatu za kisasa katika kanda zitakazoundwa baada ya utafiti.

- Serikali ya CHADEMA itaboresha Chuo Cha Polisi Moshi kwa kukipatia vifaa na nyenzo za kisasa za mafunzo ili kuweza kuhakikisha maafisa wanaondaliwa hapo wanakuwa tayari kutumika katika ulinzi na usalama nchini na kukabiliana na changamoto za uhalifu wa kisasa.

- Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa Chuo Kikuu cha Polisi Dar es Salaam kinatoa mafunzo ya kisasa ya masuala ya uhalifu, usimamizi wa sheria na haki kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za elimu ya juu nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa maafisa wa ngazi za juu wa Polisi wanaopitia chuo hiki wanakuwa na uwezo wa hali ya juu kuwaongoza maafisa wa Polisi walio chini yao.

- Lengo la serikali ya CHADEMA ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na uwiano wa polisi 1 anayehudumia watu 1000 nchini yaani (1:1000) ifikapo 2020 ili kuhakikisha kuna amani na utulivu nchini. Pamona na hilo tunatambua kuwa baadhi ya maeneo yetu yana watu wengi sana kwenye kilometa moja ya mraba. Hivyo, Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa jeshi la Polisi linazingatia uwiano wa watu kimraba vile vile. Maeneo yote yenye watu wengi yatasogezewa jeshi la Polisi kwa ukaribu zaidi. Hivyo, Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa Halmshauri za Miji na Uongozi wa Mikoa inapanga utaratibu wa kusogeza vituo vya Polisi kwenye maeneo ambayo yana idadi kubwa ya watu ili kuhakikisha usalama na amani katika maeneo hayo.

- Kuhakikisha kuwa maafisa wa jeshi la Polisi wa ngazi zote wanapata mishahara na marupurupu ambayo yanawasaidia kuondokana na vitendo vya rushwa na kuwa na nidhamu ya hali ya juu ya kijeshi.

- Serikali ya CHADEMA itaandaa mpango maalumu wa ujenzi wa makazi ya kisasa ya jeshi la Polisi kuanzia bajeti ya 2011/12 ili kuhakikisha kuwa ifikapo

mwaka 2020 maafisa wote wa Polisi wanakaa katika kambi za kisasa za jeshi ili kuongeza ushikamano (cohesion), nidhamu, na uwajibikaji wa haraka.

- Katika kuimarisha usalama mkoani Dar es Salaam, kuanzia bajeti ya 2011/2012 , Serikali ya CHADEMA itaviimarisha vituo vitatu vya Polisi kwa kuanzisha ujenzi wa majengo ya kisasa. Vituo hivi ni:
    - Kituo cha Polisi cha Kati
    - Kituo cha Polisi cha Msimbazi
    - Kituo cha Polisi cha Oysterbay
- Aidha, Serikali ya CHADEMA itaongeza vituo vinne vya kisasa jijini Dar es Salaam. Vituo hivi ni:
    - Kituo cha Polisi cha Ubungo
    - Kituo cha Polisi Kawe
    - Kituo cha Polisi cha Mbagala
    - Kituo cha Polisi Magomeni

8.2.2 Jeshi la Magereza

Hali ilivyo kwa sasa ni kwamba magereza yetu yana uwezo wa kuchukua wafungwa wapatao 22,669, lakini kuna wafungwa wapatao 45,000. Kwa hivyo uwezo wa magereza yetu ni mdogo sana ukilinganisha na mahitaji halisi. Ili kuimarisha idara ya magerezani nchini, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

- Kupitia sheria ya Magereza ya 1967 ili kuifanyia mabadiliko mbalimbali ili hatimaye kuweza kujenga jeshi la kisasa la magereza nchini. Mabadiliko hayo yataliondoa rasmi jeshi la Polisi kutoka chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani na kuliweka chini ya Wizara ya Sheria na Katiba.

- Jeshi la Magereza ndilo litakalopewa haki pekee ya kutoa ulinzi kwa majaji, mahakama na taasisi zote zinazohusiana na masuala ya mahakama kwa mujibu wa taratibu zitakazowekwa.

- Jeshi la Magereza litakuwa na idara maalum ya kufuatilia wafungwa ambao wametoroka au watu ambao wamekwepa kutimiza hukumu za mahakama. Katika hili maafisa wa magereza wakiwa wanasimamia hukumu za mahakama watapewa uwezo kisheria kuingia mahali popote, wakati wowote na kwa mtu yeyote ili kuhakikisha kuwa hukumu ya mahakama inatekelezwa.

- Serikali ya CHADEMA itapitisha katika Katiba na kufanyia marekebisho sheria mbalimbali ili ieleweke na taasisi zote na vyombo vyote vya ulinzi na usalama kuwa wakati wowote maafisa wa magereza wanatekeleza hukumu ya mahakama na wakionesha nembo za uthibitisho wa kazi zao basi hakutakuwa na mtu au chombo kingine chochote kitakachozuia utekelezaji wa kazi za maofisa wa magereza. Hili litawekwa chini ya tishio la adhabu ya kuzuia haki kutendeka (obstruction of justice) kwa mtu yeyote atakayeingilia kati kazi hizi za maafisa wa magereza.

- Chuo cha Magereza Tukuyu kitafanyiwa ukarabati mkubwa pamoja na kupatiwa nyenzo za kisasa ili kiweze kuandaa maafisa wa magereza wenye weledi wa hali ya juu na wenye kufikia vipimo vya kimataifa.

- Chuo cha Magereza Ukonga kitaboreshwa ili kiweze kutoa mafunzo ya kisasa ya masuala ya usimamizi wa magereza, masuala ya haki na usimamizi wa maamuzi ya mahakama.

8.2.3 Kikosi cha Uokoaji

Mabadiliko makubwa ya mfumo wa kikosi cha Uokoaji yatakuwa ni pamoja na kuondoa kikosi hiki kutoka katika ngazi za kitaifa kama ilivyo sasa na kuweka kazi hii katika Halmashauri za Miji na Majiji. Kila Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuunda

kikosi chake cha Uokoaji na Dharura (rescue and emergency services) ili kuhakikisha kuwa kila mji una maafisa wa kutosha na vifaa vya kutosha kukabiliana na majanga mbalimbali.

Hii itaondoa matatizo yaliyopo sasa ambapo maamuzi mengi ya idara hii yamekuwa yakitegemea maamuzi ya wanasiasa na viongozi wa kitaifa kuliko viongozi wa chini. Kutokana na unyeti wa shughuli zake vikosi vya uokoaji vitaundwa chini ya mamlaka za Halmashauri na halmashauri hizo zitasimamia mfumo, utawala na utendaji wa vikosi hivyo.

8.2.4 Idara ya Uhamiaji

Serikali ya CHADEMA itafanyia marekebisho na kuboresha idara ya uhamiaji ili kuifanya iwe ya kisasa zaidi na yenye kukidhi mahitaji ya wageni wanaoingia nchini na wananchi wanaotaka kutoka nje ya nchi. Katika kufanya hivyo:

- Serikali ya CHADEMA itaondoa ukiritimba wa upatikanaji wa hati za kusafiria kwenda nje ili kuhakikisha kuwa huduma hii inapatikana katika kila mkoa kwa haraka.

- Mikoa itatakiwa kushughulikia maombi ya hati za kusafiria kwa kushirikiana na idara ya Uhamiaji Makao Makuu ili maombi yote yawe yamefanyiwa kazi ndani ya siku 21.

- Serikali ya CHADEMA itapitisha mapema inavyowezekana katika mwaka 2011 mabadiliko ya Katiba yatakayoondoa katazo la uraia wa nchi zaidi ya moja. Hivyo, Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa hakuna Mtanzania yeyote ambaye anavuliwa Utanzania wake kwa vile amechukua uraia wa nchi nyingine. Hii ina maana kuwa Tanzania itaendelea kumtambua Mtanzania hata kama amepata uraia wa nchi nyingine isipokuwa kama mtu huyo atakuwa ameukana uraia wa Tanzania yeye mwenyewe.

- Kutokana na hilo Serikali ya Tanzania itaanzisha idara maalum ya kusimamia Raia wa Tanzania walio Nje ya Nchi - Tanzanian Citizens Abroad- ambao watatambulika kuwa ni wananchi wote wa Tanzania pamoja na uzao wao. Watoto watakaozaliwa au ambao wamezaliwa na Watanzania k nje ya nchi na wamefikisha miaka 18 wataweza kuomba pasi za kusafiria za Tanzania.

- Serikali ya CHADEMA itaanzisha utaratibu wa kuwatumia Watanzania walio nje ya nchi katika kutoa mchango wa ujenzi wa taifa kwa utaratibu ambao utawekwa. Lengo ni kuweza kuchota na kutumia ujuzi na utaalamu mbalimbali uliopo katika wananchi hao. Serikali ya CHADEMA itaanda kongamano la kwanza la kimataifa la raia wa Tanzania nje ya nchi ngwe ya pili ya mwaka 2011 ili kutoa nafasi kwa Watanzania hao kuweza kubadilishana mawazo na utaalamu na Watanzania wenzao walio nyumbani.

8.2.5 Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa

Kwa vile jeshi la nchi yoyote ndio ngao inayoonekana ya ulinzi wa nchi hiyo basi jukumu la JWTZ haliwezi kuchukuliwa na chombo kingine chochote. Hivyo Serikali ya CHADEMA ikitambua nafasi ya pekee ya ulinzi wa taifa letu ambayo inashikiliwa na JWTZ itahakikisha kuwa jeshi hili linakuwa ni la kisasa, la haraka, lenye nguvu na liko tayari wakati wote kulinda nchi yetu na mipaka yake.

Ili kuimarisha zaidi Jeshi letu la Ulinzi na Usalama, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

- Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa ujenzi wa kambi za kisasa za Jeshi unafanyika ili ifikapo 2015, wapiganaji wetu wote wanaishi katika kambi za kisasa na katika nidhamu ya kijeshi na utayari wa kivita.

- Jeshi letu litaongozwa na nadharia mpya ya kivita ambao msingi wake ni “Ulinzi wa Nchi Yetu” (defending our homeland!) Nadharia hii itaongoza utendaji wa

vikosi vya kijeshi ili kuhakikisha kuwa Tanzania kweli inakuwa huru dhidi ya maadui wa ndani na wa nje.

- Tutaboresha idara ya Kijasusi ya Jeshi ili iweze kushirikiana na idara za kiraia ili kuweza kubadilishana taarifa mbalimbali zenye kutishia taifa letu.

- Tutaanza mchakato wa ununuzi wa meli kubwa mbili za kivita ambazo zitaongoza ulinzi wa mipaka yetu ya bahari pamoja na meli ndogondogo. Kwa kushirikiana na washirika wetu wa maendeleo wa kimataifa tutahakikisha jeshi letu la majini (Navy) lina uwezo wa kuzuia uharamia na uvamizi wa majini.

- Tutaondoa kikosi cha Polisi cha Majini (Police Marine) na kutokana nacho tutaunda kikosi kipya cha Ulinzi wa Pwani na Fukwe (Tanzania Coast Guard). Kikosi hiki ndicho kitakachokuwa na nguvu za kipolisi katika maeneo ya pwani na fukwe za maji yetu katika bahari ya Hindi na maziwa yetu pamoja na mito mikubwa. Tutapatia kikosi hiki zana mbalimbali na vitenda kazi vya kisasa. Mpango wa kuundwa kwa kikosi hicho utaanza kufanyiwa upembuzi yakinifu katika bajeti ya 2011/2012 na utekelezaji wake kuanzia mapema 2012 ili hatimaye ifikapo 2014 Kikosi hiki kiwe tayari kuanza kazi kama Jeshi la Ulinzi wa Pwani na Fukwe. Kikosi hiki kitapewa jukumu la kusimamia uhalifu unaofanyika majini usiohusiana na masuala ya mapigano ya kivita.

- Serikali ya CHADEMA inakusudia kurudisha utaratibu wa kutumikia Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria ili kurudisha moyo wa utumishi, kujitokea na ujenzi mpya wa taifa. Serikali ya CHADEMA itaandaa utaratibu utakaowalazimu viongozi na watumishi wa umma kupitia mafunzo ya muda mfupi katika Jeshi la Kujenga Taifa yatakayolenga katika kuchochea uzalendo, maadili na uadilifu katika utumishi wa umma.

- Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na JKT yataongozwa na falsafa ya kushiriki katika ujenzi wa taifa wakati wa amani na kuwa tayari katika ulinzi wa taifa. Mipango yetu mingi ya ujenzi mpya wa taifa letu itatumia kwa kiwango cha juu kinachowezekana, utaalamu, utayari na uwezo wa majeshi haya.

- Serikali ya CHADEMA itaweka jukumu la ujenzi na usimamizi wa baadhi ya miundo mbinu chini ya Kikosi cha Uhandisi cha Jeshi (TPDF Engineers Corps). Kwa vile kuna utaalamu mkubwa katika masuala ya ujenzi ndani ya jeshi hilo, tunaamini ni kukosa ubunifu kutokuwatumia katika ujenzi wakati wote wa amani na siyo wakati wa dharura tu.

8.2.6 Idara ya Usalama wa Taifa

Kama Jeshi la Wananchi ni alama ya wazi ya ulinzi wa taifa basi Idara ya Usalama wa Taifa ni alama isiyoonekana ya ulinzi huo. Tunaweza kusema kwa uhakika kabisa kuwa Idara ya Usalama ya Taifa ndiyo mlinzi wa kwanza kabisa katika taifa lolote, na hivyo kulegalega kwa idara hii ni kuhatarisha usalama wa nchi.

Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na migongano ya maslahi mbalimbali ndani ya Idara hii kiasi kwamba morale wa utendaji kazi na motisha umekuwa ukifuatana na maslahi ya kisiasa ya viongozi mbalimbali. Weledi umepungua na utii kwa nchi uko matatani. Hali hii haiwezi kuachwa kuendelea kama kweli tunataka kujenga uchumi na maisha ya kisasa.

Idara ya Usalama wa Taifa inatakiwa kuwa ndiyo chombo ambacho kinaweza kukusanya taarifa za kijasusia na hata kuzuia matukio mbalimbali kabla hayajatokea. Tumeshuhudia kwa miaka zaidi ya kumi na tano sasa idara hii ikiwa imemomonyolewa na kuvurugwa kwa maamuzi ya kisiasa na hivyo kuifanya ibakie kama isiyo na uongozi na uelewa wa kisasa wa majukumu yake. Serikali ya CHADEMA itasahihisha tatizo hili mara moja kwa kuchukua hatua zifuatazo:

- Kufanyiaa mabadiliko sheria iliyounda Usalama wa Taifa (TISS) ya 1996 sasa ili kuunda chombo kipya kitakachosimamia masuala ya Inteligensia nchini.

- Katika mabadiliko hayo Wakala wa Usalama wa Taifa **(National Intelligence Agency)** utaundwa na kuwa ndicho chombo cha juu kabisa cha masuala ya intelligentsia nchini. Chombo hiki ndicho kitaratibu ukusanyaji, uchambuzi,

ugawaji na ufuatiliaji wa taarifa mbalimbali za kijasusi. Mkurugenzi Mkuu wa NIA atapendekezwa na Rais na kupitishwa na Bunge.

- Idara zote hizo za chini ya NIA zitaongozwa na Wakurugenzi ambao watateuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge.

- Makao Makuu ya NIA yatajengwa huko Kigamboni na idara hiyo itakuwa huru kutoka Ikulu. Ujenzi wa Makao Makuu ya Idara hii yatafanywa kwa kushirikiana na Idara ya Uhandisi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vyombo vingine vya Usalama.

- Tutapitia mfumo wa mafunzo na upatikanaji wa watumishi wa NIA ili kuhakikisha kuwa wanaoingia katika idara ya Usalama wa Taifa ni wale tu ambao watakuwa wamewahi kupitia vyombo vya kijeshi na wale ambao watakuwa wameshaajiriwa bila mafunzo hayo kuhakikisha wanapitia mafunzo ya kijeshi kwa utaratibu utakaowekwa.

SURA YA TISA

9. KUKUZA NAFASI YA TANZANIA KATIKA DIPLOMASIA YA KIMATAIFA

9.1 Utangulizi

Miongo kadhaa iliyopita Tanzania ilikuwa inajulikana duniani kwa misimamo ya kimantiki na katika kuendesha na kuunga mkono harakati za ukombozi wa wanyonge popote duniani. Aidha Tanzania ilitia mkazo kwenye sera ya kujitegemea isiwe taifa ombaomba. Ni kutokana na misimamo ya kimantiki Tanzania iliweza kujulikana na kuheshimika kimataifa. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni, Serikali ya CCM imeharibu misingi ya mahusiano ya kimataifa iliyojijengea nchi yetu sifa za kuwa huru katika mhusiano yake na nchi za nje. Badala yake, sera ya CCM kuhusu ushirikiano wa kimataifa imelenge katika kuiwezesha Tanzania kuomba misaada kutoka nchi zilizoendelea na hata zile ambazo sio muda mrefu zilikuwa zikiongozwa na Tanzania katika harakati za kudai mfumo mpya wa ki-uchumi ulimwenguni. Matokeo yake kwa sasa nchi yetu inajulikana zaidi jinsi ilivyoombaomba na kuwa moja ya nchi maskini zaidi duniani.

9.2 Lengo la CHADEMA kuhusu ushirikiano wa kimataifa ni kuhuisha nafasi ya Tanzania katika jumuiya ya kimataifa katika kukomesha uonevu na ukandamizaji na kuchochea utawala bora na ukuaji wa demokrasia, hasa katika nchi za kiafrika. Aidha lengo la CHADEMA ni kubuni mikakati ya makusudi ya kuijengea Tanzania nafasi mpya katika uchumi wa ulimwengu. Serikali ya CHADEMA itajenga mahusiano ya kidiplomasia yanayolenga kubadilisha na kukuza uchumi wake.kwa kushirikiana na nchi kama China na nchi zingine za bara Asia zilizoonyesha maendeleo ya kasi katika kipindi cha karibuni..

Katika kutimiza adhima ya kujiendeleza katika sekta ya sayansi na teknolojia, Serikali ya CHADEMA itaweka mkazo katika kuimarisha mahusiano yanayolenga kuiwezesha Tanzania kuiga na kuchota maendeleo ya kiteknolojia yaliyofikiwa katika nchi za Asia na hasa China.

9.3 Serikali ya CHADEMA itahuisha juhudi za Tanzania za kuhakikisha kuwa bara la Afrika linaungana kijamii, kiuchumi na kisiasa kama walivyoazimia waasisi wa bara hili, Mwalimu Nyerere na Kwame Nkrumah. CHADEMA inaamini kwamba suala la umoja wa Afrika ni la msingi na ulazima katika maendeleo ya nchi zetu hasa katika hali ya utandawazi inayohitaji nguvu ya pamoja ili kulinda maslahi ya mwafrica na kunufaika na rasilmali za bara hili.

Aidha, CHADEMA inaamini kuwa Tanzania inayo nafasi kubwa na ya kipekee katika Afrika ya Mashariki na hivyo ina nafasi muhimu katika kuhakikisha kuwa malengo ya ushirikiano yanafikiwa. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni Tanzania imepata sifa ya kusitasita na imepoteza uongozi wake wa ki-historia katika katika kanda hii. Tutarejesha nafasi hiyo kwa kujenga ujasiri wa Watanzania katika kukabili changamoto za ushirikiano. Hivyo, Chadema, badala ya kusema kwamba hatuko tayari kila kukicha itabuni na kusimamia mikakati ya kuiweka Tanzania kuwa kiongozi katika kuhitimisha lengo la kufikia Shirikisho la Afrika Mashariki.

SURA YA KUMI

10. KUINUA NA KUKUZA SANAA, MICHEZO NA UTAMADUNI

10.1 Utangulizi

Kila taifa duniani linajitofautisha na linatofautishwa na sanaa zake, michezo na utamaduni wake. Japo mataifa yanafanana katika mambo kama ya ujuzi na matumizi ya sayansi na teknolojia na hata miundo mbalimbali ya tawala zake linapokuja suala la sanaa, michezo, na utamaduni kila taifa linajitahidi kulinda kile kitu ambacho ni “chake”.

Baba wa Taifa alituusia sana katika kulinda na kuendeleza utamaduni wetu kwani ndio unatufanya tuwe ‘Watanzania’ na Waafrika. Tunatambua kabisa kuwa jamii yetu ni mchanganyiko mzuri wa tamaduni mbalimbali za kiafrika, kiasia, kiarabu na za ulaya magharibi. Hata hivyo tunatambua vile vile kuwa sisi ni taifa la kiafrika na kwa hilo tunajivunia na tunaona fahari na tutakuwa tayari kulilinda kwa ajili yetu sisi wenyewe na kwa ajili ya watoto wetu.

Lengo la Serikali ya CHADEMA ni kuhakikisha kuwa utamaduni na sanaa ya Mtanzania inatunzwa na kuendelezwa pasipo kuwa na hisia ya uduni, aibu au kwa namna yoyote kuiona ni “ya kizamani”. Katika kukamilisha lengo hili, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo:

10.2 Sanaa

- Kubadilisha Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo na kuwa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Kawawa cha Bagamoyo (Kawawa Memorial University - Bagamoyo). Chuo hiki kitatoa mafunzo yote ya juu ya mambo ya sanaa, michezo

na tamaduni kwa vijana wa Kitanzania na wale wanaotoka ng'ambo. Mchakato wa kukiinua Bagamoyo kuwa Chuo Kikuu utakamilika ifikapo 2012.

- Kuhakikisha masomo ya Sanaa yanarudishwa katika ngazi zote za elimu ili kuwakoleza vijana wetu katika ubunifu na umahiri wa kazi za sanaa na kuinua vipaji vyao mbalimbali. Shule zote za umma na za binafsi zitatakiwa kuwa na masomo ya Sanaa mbalimbali.

- Mafunzo ya Sanaa katika vyuo vya elimu yatatolewa ili kuwaandaa walimu wa masomo hayo.

- Mashindano ya Sanaa katika mashule yatakuwa ni sehemu ya mashindano ya michezo ya UMISHUMTA na UMISETA.

- Tutahakikisha kuwa asilimia 90 ya bajeti zote za wizara, idara, taasisi na wakala wa serikali zinazotengwa kwa ajili ya kunaksisha ofisi zinatumia kazi za sanaa na samani zinazopatikana Tanzania au zinazotokana na ubunifu wa Watanzania. Hii itachochea ajira katika kazi za sanaa na ushindani wa kibiashara ambao utainua ubora wa kazi hizo.

- Maslahi ya wasanii nchini yataboreshwa kwa kutengeneza taratibu za kisheria zitakazolinda kazi zao mbalimbali za sanaa, haki zao za ubunifu na kuheshimu vipaji vyao. Tutasimamia vikali kabisa unyonyaji wowote wa kazi za msanii na mtu yeyote au chombo chochote ambacho kitathibitika kuwa kinawanyanyasa wasanii au kutumia kazi za wasanii kiubaguzi au upendeleo usio na msingi wa ushindani wa kibiashara au haki basi atachulikwa hatua kali za kisheria ikiwemo

kupoteza leseni, faini kubwa na hata kifungo. Chini ya Serikali ya CHADEMA kazi za wasanii zitalindwa na watajua na kuona zinalindwa na watanufaika nazo.

10.3 Michezo

Michezo ni mojawapo ya vitu ambavyo vinawaunganisha watu kwa haraka zaidi na ni tunu ambayo inajenga ujirani mwema, urafiki, umoja na udugu. Lakini vile vile michezo ni afya na zaidi ya yote michezo ni ajira . Kwa muda mrefu michezo hapa nchini imekuwa ikichuliwa kama burudani tu vitu vya kujifurahisha pasipo kupata umuhimu wake unaostahili. Chini ya Serikali ya CHADEMA sekta ya michezo itakuzwa ili kuhakikisha kuwa michezo ni zaidi ya burudani na kujifurahisha bali kuwa ni sehemu ya kuchochea ajira na kuchangia katika shughuli za kiuchumi. Ili kuweza kukuza michezo, serikali ya CHADEMA:

10.3.1 Itahakikisha kuwa elimu ya michezo inatolewa katika Chuo Kikuu cha Kawawa cha Bagamoyo ili kuweza kupata wataalamu wa Sanaa na Michezo waliobobea katika elimu. Hii itakuwa ni pamoja na kuandaa shahada za ufundishaji michezo mbalimbali ili taifa liweze kujipatia wataalamu wa ndani na kuacha kwenda kutafuta watalaamu kutoka nje, kitu ambacho hatujaweza kuonesha mafanikio yake kwa zaidi ya miaka arobaini sasa.

10.3.2 Katika bajeti ya Wizara ya Michezo na Utamaduni ya 2011/2012 Serikali ya CHADEMA itatenga fungu la fedha ili kutoa nafasi kwa vijana wetu na watalaamu wetu ambao wangependa kwenda kusomea mafunzo ya juu ya michezo ili waweze kuwa na uwezo mkubwa wa kufundisha timu zetu. Timu zote za ngazi za juu zitapewa nafasi ya kupendekeza majina ya wataalamu wake.

10.3.3 Ili kuirudisha Tanzania katika ramani ya dunia ya michezo, Serikali ya CHADEMA itachukua hatua mahsusi mbili zifuatazo:

i) Kuhakikisha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika mashindano ya Olimpiki ya London 2012. Hivyo, ndani ya siku sitini (60) tu baada ya kuingia madarakani serikali ya CHADEMA itaunda timu itakayosimamia maandalizi ya timu ya Taifa ya Olimpiki ili kuhakikisha kuwa tunaweka lengo la kurudi na Medali zisizopungua 20 katika mashindano mbalimbali huko London. Lengo letu itakuwa ni kuandaa kikosi cha wanariadha 200 watakaoshiriki mashindano mbalimbali huko London na hatimaye kuweka jina la Tanzania katika medani za michezo.

ii) Kufanya maandalizi kabambe ya timu ya Taifa ya Soka ya wanaume ili iweze kushiriki mashindano ya Kombe la Dunia 2014 huko Brazili. Japo ndoto hii yaweza isionekane inayowezekana CHADEMA inaamini kwa ushirikiano mzuri wa kada mbalimbali, kujitolea na mfumo mzuri wa mafunzo na mazoezi Tanzania inaweza kabisa kuinuka kwa mwendo wa kasi. Katika kutekeleza hili, CHADEMA imeandaa mpango madhubuti wa kitaalamu wa kuandaa timu hiyo ya taifa na mpango huo utaanza kutekelezwa ndani ya miezi sita baada ya serikali ya CHADEMA kuingia madarakani. Watanzania wakitupa hatamu ya uongozi wa nchi yetu tunawaahidi kuwa katiks kombe la dunia la 2014 Tanzania itakuwa mshiriki. Tunaamini hili haliwezi kutokea kwa kuombea au kunuia bali kwa mipango kamambe, uongozi imara na mikakati ya makusudi ambayo CHADEMA imekuwa ikiiandaa kwa karibu miaka miwili sasa. Ramani ya kwenda Brazili iko tayari, tunachosubiri ni ridhaa ya Watanzania kuanza kuitekeleza.

10.3.4 Ili kujenga uhusiano bora na ndugu zetu wa Afrika ya Mashariki tutahakikisha kuwa mashindano ya michezo mbalimbali baina ya timu zetu mbalimbali na zile za majirani zetu yanafanyika mara kwa mara ili kujenga udugu, na ujirani mwema.

10.3.5 Tutarudisha mashindano ya mashirika na taasisi za umma na kuyaboresha zaidi ili yawe na mvuto kwa kutoa zawadi nono pamoja na kuvutia wadhamini mbalimbali. Michezo ya Majeshi nayo itaboreshwa ili kuzidi kupata wachezaji bora tunapojiandaa na London 2012.

10.3.6 Shule zote za Sekondari na Vyuo vyote vinavyopata usajili vitatakiwa katika mipango yao yote kuwa na maeneo ya michezo ya nje na ya ndani. Kutokana na hili tutaanzisha na kuboresha mashindano ya michezo ya Vyuo Vikuu vyote nchini ili huko nako tuweze kupata wachezaji mbalimbali na vile vile kujenga uhusiano wa karibu katika ya vyuo na vyuo.

10.3.7 Tutaweka utaratibu wa kisheria ili kusimamia ajira za sekta ya michezo ikiwemo mikataba ya wachezaji, maslahi yao na mafao yao. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa wachezaji wote wanaopata nafasi ya kuchezea ngazi za ligi za kitaifa au kuwakilisha taifa wanapata malipo ya ajira na mafao kama watumishi wengine wa umma. Hii itasaidia katika kuhakikisha kuwa michezo inapata watu walio bora na ambao wananufaika na ajira katika michezo bila hofu ya kutojua maisha yao yatakuwaje baada ya umri wao wa michezo kupita. Tutahakikisha sheria hii inalinda maslahi ya wanamichezo wote nchini na kuhakikisha wale wanaojiriwa

katika michezo wanapata maisha yao kwa njia hiyo na kwa haki na mafao ya uzeeni.

10.4 Kuunda Kamisheni Maalumu ya Rais ya Historia ya Tanzania

Kwa vile tunaishi katika kipindi muhimu cha mpito wa historia tangu kizazi cha uhuru na kile kilichozaliwa baada ya Uhuru ni muhimu kuhakikisha kuwa historia yetu inakusanywa, kuchambuliwa na kutunzwa vizuri kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Hivyo Serikali ya CHADEMA kuunda *Kamisheni Maalum ya Rais ya Historia* ambayo, pamoja na mambo mengine itakuwa na majukumu yafuatayo:

- Kufanya utafiti wa watu wote waliotoa mchango mkubwa wa kihistoria katika Uhuru wa Tanganyika, Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano ili waweze kukumbukwa na michango yao kuenzeiwa
- Kutambua maeneo, majengo, na sehemu mbalimbali zenye umuhimu mkubwa wa kihistoria
- Kupitia matukio muhimu ya historia yetu ili yaweze kuelezewa katika mwanga wa kihistoria. Hii ni pamoja na Uhuru, Mapinduzi, Muungano, Uasi wa Jeshi, Azimio la Arusha, Operesheni Vijijini na Vita ya Kagera
- Kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuenzi watu mbalimbali ambao walichangia katika matukio mbalimbali kwa namna ya pekee na ambao historia yetu haijawakumbuka ipasavyo.
- Kukusanya vielelezo mbalimbali vyenye umuhimu mkubwa wa kihistoria kutoka watu binafsi, taasisi binafsi na nje ya nchi ili hatimaye vitu hivyo viweze kuingizwa katika historia yetu kwa ajili ya kuwa ni urithi wa vizazi vijavyo.
- Kuandika ripoti maalum juu ya historia yetu na matukio mbalimbali ili yaweze kutunzwa kama sehemu ya historia yetu maalum

SURA YA KUMI NA MOJA

11. VIPENGELE MAALUM

11.1 Zanzibar na Muungano

Serikali ya CHADEMA ina mpango madhubuti kabisa wa kuimarisha Muungano na kuhakikisha kuwa kero zote za Muungano zinaondolewa katika mwaka wa kwanza na kuachana na utaratibu wa kimazingaombwe unaofanywa na serikali ya CCM na kutishia Muungano wetu. Serikali ya CHADEMA itachukua hatua zifuatazo katika kuiwekea mazingira mazuri kwa maendeleo na katika kuimarisha Muungano:

- Suala la mafuta litaachwa mikononi mwa Serikali ya Zanzibar hasa tukizingatia kuwa visiwa hivi vina raslimali ndogo sana za kiuchumi. Masuala ya raslimali nyingine yatajadiliwa ili kuhakikisha kuwa Zanzibar inanufaika na raslimali za Tanzania na vile vile inatoa mchango wake sahihi katika uchumi wa taifa.

- Serikali ya CHADEMA itaitisha mkutano maalum wa pamoja wa Baraza la Wawakilishi na Bunge la Muungano na wadau wengine ili hatimaye kukaa chini kama ndugu wamoja na kujadili masuala yenye matatizo yanayohusu Muungano. Kutakuwa na kikao cha Pamoja cha Uongozi wa Taifa mara mbili kwa mwaka.

- Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa vikwazo mbalimbali ambavyo vinaonekana kutatiza ufanyaji wa biashara na uwekezaji katika visiwa hivyo vinaondolewa.

11.2 Unguja

Kwa vile Unguja ni eneo la kihistoria na historia yake imefungamana kabisa na historia ya Tanzania bara na pwani ya mwambao juhudi za wazi zitafanyika ili kulinda tunu hiyo ya kihistoria. Hii ni pamoja na:

- Kufanya ukarabati wa majengo na maeneo ya kihistoria yaliyoko Unguja ili kuhakikisha yanaingizwa na kutunzwa katika mfumo wa kisasa ili yaendelee kuwa ni urithi kwa vizazi vijavyo.

- Kwa kushirikiana na serikali ya Zanzibar, tutatenga eneo eneo jipya kwa ajili ya ujenzi wa Jiji la Kisasa la Zanzibar (Zanzibar City) kwenye eneo ambalo litakubaliwa na Serikali ya Zanzibar ili hatimaye kujenga jiji la kisasa visiwani humo ambalo litakuwa ni kitovu cha utalii wa maeneo ya kisasa na yale ya kihistoria.

11.3 Pemba

Mji wa Pemba ni mji ambao bado haujaingizwa vizuri kabisa katika uchumi wa nchi na umeendelea kubakia mahali penye kuahidi mafanikio bila kuyatoa. Chini ya Serikali ya CHADEMA Pemba itatengwa maalumu kuwa kitovu cha biashara ya mambo ya fedha (Financial Centre) ili kushindana na maeneo kama ya UAE, Saudi Arabia, Qatar n.k Lengo letu ni kuhakikisha kuwa Pemba inakuwa ni makao makuu ya taasisi mbalimbali za kifedha na makampuni mbalimbali. Ili kutimiza adhma hii

- Kuanzia Bajeti ya 2011/2012 upembuzi yakinifu utafanywa ili kuona ni jinsi gani mkongo wa mawasiliano ambao unapita katika bahari ya Hindi unaweza kuchepushwa kuelekea Pemba na hivyo kuipatia Pemba njia za ‘fibre optics’ na kurahisisha mawasiliano.

- Kwa kushirikiana na Serikali ya Zanzibar utawekwa mfumo maalum wa kodi mbalimbali kwa ajili ya Pemba kuwa kivutio cha uwekezaji wa taasisi za fedha. Lengo ni kufanya Pemba kuwa ni eneo la unafuu wa kodi (Tax Haven) kwa makampuni ya ndani na ya kimataifa. Ili kuhakikisha hili linafanikiwa tutahakikisha kunakuwepo na umeme wa kudumu, huduma safi ya maji, tiba na udhibiti wa kisasa ili kuhakikisha kuwa Pemba haitotumiwa na wahalifu wa kimataifa katika masuala ya kodi.

- Kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Serikali ya Muungano itahakikisha kuwa miji ya Chake Chake na Wete inapatiwa ujenzi wa majengo ya kisasa pamoja na miundo mbinu ya kisasa na huduma za kuaminika za usafiri kati yake ya Tanga.

11.4 Mpango wa CHADEMA kuhusu Wanawake na Watoto

Mpango madhubuti wa kuinua maisha ya wanawake utafanyika na utahakikisha kuwa wanawake wa Tanzania wanapata nafasi sawa za kufanikiwa. Hii ni pamoja na kufanyia marekebisho sheria mbalimbali ili kuweka usawa wa kisheria. Zaidi ya yote utaratibu wa ajira utahakikisha unazawadia matokeo (meritocracy) ili kutoa nafasi kwa wanawake wanaofanya vizuri katika kazi na fani zao kuweza kupanda vyao kwa haki bila kuonewa au kupitwa. Pamoja na hayo yote, Serikali ya CHADEMA:

- Itahakikisha kuwa unyanyasaji wa wanawake katika masuala ya miradhi na talaka unakoma. Kwa kushirikiana na taasisi za kidini na kijamii tutahakikisha kuwa masuala ya mirathi nchini yanasimamiwa katika mtindo wa kisasa wenye kuheshimu haki mbalimbali za wanandoa bila kuingilia taratibu za kidini pale ambapo mwanamke ameamua masuala yake kuendeshwa kwa misingi hiyo.

- Haki za watoto zitazingatiwa ikiwepo haki ya kuishi katika mazingira ya amani, kusoma na kuwa mtoto. Hili hata hivyo litahakikisha kuwa haki za wazazi kulea watoto wao zinalindwa na kuheshimiwa na watu wote na serikali pasipo sababu kubwa na ya msingi haitangilia malezi ya watoto katika familia zao.

- Tutahakikisha vyombo vya burudani vinaheshimu haki za familia kulea watoto wao pasipo kuwasukumizia watoto burudani ambazo zimekusudiwa kwa watu wazima. Hii ina maana ya kwamba burudani mbalimbali zinazofanywa zenye maudhui ya kiutu uzima zitatakiwa kuhakikisha kuwa watoto hawaruhusiwi kushiriki burudani hizo na wale watakaokiuka watakabiliwa na adhabu kali. Hii ni pamoja na burudani za muziki, vileo, na uvutaji wa sigara. Katika hili Serikali ya CHADEMA itakuwa ni mtetezi na msimamizi wa maadili bora ya watoto. Adhabu kali zitatolewa kwa vyombo vya habari ambavyo vitakiuka kanuni za maadili ikiwemo pamoja na faini, kunyang’anywa leseni na hata vifungo kwa wamiliki wake.

- Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa mtu yeyote mzima atakayethibitika kuwa amemtia mimba mtoto anaadhibiwa vikali na analazimishwa kulipia gharama ya ujauzito na malezi ya mtoto huyo hadi mtoto anapofikia miaka 18. Hivyo tutaweka

utaratibu ili wasichana au familia za wasichana hao ambao wamepata uja uzito katika umri mdogo kuweza kufungua kesi za madai au za uhalifu dhidi ya wale waliowapatia mimba hizo.

- Tutahakikisha kuwa sheria inawekwa ili kulazimisha mtu yeyote mwenye ugonjwa wa zinaa, ikiwemo UKIMWI, kumwambia mwenzi wake mapema ili kumpa nafasi ya kuamua na kujikinga kabla ya mahusiano ya kingono kuanza. Endapo mtu anajijua kuwa ameambukizwa ugonjwa wa zinaa na hatatoa taarifa kwa mtu mwingine basi endapo itathibitishwa kuwa amemwambukiza mwenzake basi itachukuliwa ni kitendo cha makusudi na ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria. Tutajifunza katika nchi nyingine jinsi ya kuandika sheria ambayo inaendana na mazingira yetu vile vile na yenye kuheshimu utu, usiri na haki za mtu.

- Serikali ya CHADEMA itaandaa na hatimaye kupitisha Sheria yenye kuzuia na kukabiliana na matumizi ya nguvu majumbani na ya vuguru za kijinsia (Gender Based Violence Act). Licha ya kutungwa kwa sheria hiyo, kutakuwa na hatua nyingine ambazo zitachukuliwa ili kukabiliana na tatizo hili ambalo ni kubwa katika jamii yetu. Hatua hizi ni pamoja na:

    - Kufanyia mabadiliko sheria ya Ndoa ili kuhakikisha kuwa ubakaji ndani ya ndoa unatambulika kuwa ni kosa la jinai.

    - Kufanya mabadiliko katika sheria husika ili Kutambua vitendo vya ubakaji au matumizi ya nguvu baina ya watu wanaoishi pamoja kama wenzi na ambao hawajafunga ndoa rasmi.

    - Kulinda watumishi wa ndani na wasaidizi wa majumbani dhidi ya matumizi ya nguvu na unyanyasaji wa kijinsia.

11.5 Kujiandaa kwa Majanga

Tukitambua kuwa taifa lisilojiandaa kwa majanga linajiandaa kwa maafa, CHADEMA inatambua udhaifu mkubwa ambao umeonesha na serikali ya CCM kwa muda mrefu sasa kuandaa mfumo na utaratibu mzuri wa kukabiliana na majanga na hivyo kusubiri hadi

majanga yatokee ndiyo waanze kufikiria nini cha kufanya. Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa Tanzania inajiandaa kwa majanga makubwa na madogo na kuweka mfumo mzuri wa kukabiliana na majanga. Hii ni pamoja na:

- Kutunga sheria mpya ya ujenzi na viwango vya ujenzi vyenye hadhi ya kimataifa. Hii ni pamoja na kuangalia taratibu za ujenzi wa majumba na majengo nchini.
- Kuandaa mfumo wa awali wa kutahadharisha umma juu ya ujio wa majanga (Emergency Alert System) kwa kutumai vyombo na nyenzo mbalimbali ili kuepusha madhara makubwa kwa watu na mali.
- Kutengeneza utaratibu kuanzia ngazi za chini kabisa kwenye jumuia wa kutoa mafunzo kwa watu watakaojitolea kukabiliana na majanga.
- Kwenye miji yote mikubwa mtandao wa mabomba ya maji ya dharura utaboreshwa ili kuhakikisha kuwa miji na makazi ya watu yanafakiwa na maji ya kuzuia moto kwa haraka.

HITIMISHO: ILANI YA MABADILIKO

Ilani hii ni ilani ya mabadiliko; ni ilani yenye malengo ya kulibadilisha taifa letu kutoka katika hali yake ya sasa na kutuelekeza kwenye kuwa katika nafasi ya mafanikio. Ni ilani inayozingatia ukweli kuwa Watanzania nao wanayo haki ya kuishi maisha ya kisasa yenye kuheshimu na kulinda utu wao. Ilani hii inawezekana kutekelezeka kwani imezingatia uwezo wa ndani wa nguvu kazi, akili, vipaji, na uwezo wa kuongoza wa Watanzania wenyewe. CHADEMA inaamini kabisa kuwa endapo uongozi thabiti wenye maono makubwa ya mabadiliko unashika madaraka nchini basi kazi ya ujenzi mpya wa taifa letu itaanza upya kwa namna na mtindo ambao utalibadilisha taifa letu kwa haraka zaidi kuelekea mafanikio ya kweli na ya kudumu.

Kuanzia uongozi wa kisiasa hadi uongozi wa kitaalam CHADEMA iko tayari kuhakikisha kuwa ilani hii inageuza maisha ya Watanzania kutoka katika umaskini kuelekea mafanikio. Hivyo, CHADEMA imesimamisha wagombea kuanzia ngazi za udiwani, Ubunge na Rais na ni kwa kuwachagua hawa wote ndipo serikali makini, yenye maono ya kisasa na yenye uwezo wa kuongoza kufikia malengo makubwa na ya kuthubutu itaweza kuundwa.

Hatuhitaji chama kile kile, chenye viongozi wale wale, wenye sera zile zile zilizoshindwa. Hatuwezi kuendelea kuongozwa na nadharia kuwa maendeleo ni “wingi wa vitu” kama ambavyo serikali imekuwa ikifanya. Serikali ya CHADEMA itaweka mkazo katika maendeleo ya watu na kuhakikisha kuwa maendeleo ya vitu yanakuwa kwa ajili ya maendeleo ya watu.

Kwa kuchagua CHADEMA kuanzia udiwani, ubunge na Urais, Watanzania watakuwa wanachagua mabadiliko, watakuwa wamechagua ubora, watakuwa wamechagua maendeleo. Na sisi CHADEMA tunaahidi kuwa tutakapoingia madarakani tutafanya kazi mchana na usiku kuhakikisha kuwa njozi ya mafanikio ambayo imeanishwa kwenye ilani hii inakuwa ni ya kweli na inadumu.

Chagua Mabadiliko; Chagua CHADEMA, Tumaini Jipya

MUNGU IBARIKI TANZANIA